**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

# HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI - OFISI YA RAIS - KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA

**DKT. MWAL. HAROUN ALI SULEIMAN (MBM)**

**KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

**MEI, 2026**

**YALIYOMO**

**SEHEMU YA KWANZA ........................................................... 1**
**1.0 UTANGULIZI........................................................................ 1**
1.1 Salamu za Pongezi ................................................................ 1
1.2 Mafanikio ya Wizara katika Mwaka wa Fedha 2025/2026...... 3
Sekta ya Sheria............................................................................ 3
Sekta ya Utumishi ....................................................................... 5
Sekta ya Utawala Bora................................................................ 7
1.3 Changamoto Zilizopo na Hatua Zilizoendelea Kuchukuliwa .... 7

**SEHEMU YA PILI........................................................................ 9**
**2.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA FEDHA 2025/2026 ............................................................................. 9**
2.1 Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ..... 9
2.2 Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ........................ 9
2.3 Vipaumbele vya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ..... 10
2.4 Malengo Makuu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ................................................................ 10
2.5 Utekelezaji wa Malengo ya Ofisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ................................................................ 11
2.6 Utekelezaji kwa kuzingatia Usawa wa Kijinsia ...................... 11
2.7 Utekelezaji wa Bajeti kwa Mafungu na Programu .................. 13
2.7.1 Fungu G01: Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora............................................... 13
2.7.2 Fungu G02: Programu ya Usimamizi waUpatikanaji wa Haki ........................................................................... 25
2.7.3 Fungu G03: Programu ya Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Sheria .................................................................... 27
2.7.4 Fungu G04: Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa Kesi za Jinai.............................................................................. 29

2.7.5 Fungu G12: Programu ya Haki na Uwezeshaji Kishariah... 31
2.7.6 Fungu G14: Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini.. 32
2.7.7 Fungu G15: Programu ya Usimamizi wa Maadili ya Viongozi. 33
2.7.8 Fungu E04: Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma ........................................ 35
2.7.9 Fungu E05: Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu Uchumi........................................ 36
2.7.10 Fungu E07: Programu ya Usimamizi wa Watumishi wa Umma ........................................................ 37
2.7.11 Fungu E08: Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa Watumishi Serikalini ................................ 38

**SEHEMU YA TATU ........................................................ 40**
**3.0 MUELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA FEDHA 2026/2027 ........................................................ 40**
3.1 Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 40
3.2 Malengo Makuu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 ........................................................ 41
3.3 Malengo ya Utekelezaji kwa Programu za Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 .................................... 41
3.3.1 Fungu 005: Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora............................................... 42
3.3.2 Fungu 026: Programu ya Usimamizi na Upatikanaji wa Haki - Mahkama Kuu Zanzibar........................................ 48
3.3.3 Fungu 027: Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma - Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ................................................ 49
3.3.4 Fungu 028: Programu ya Mageuzi ya Utoaji wa Huduma za Sheria- Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali .......... 50
3.3.5 Fungu 029: Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa Kesi za Jinai - Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka .................... 51

3.3.6 Fungu 035: Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu Uchumi - Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar ............................................ 51
3.3.7 Fungu 036: Programu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma - Kamisheni ya Utumishi wa Umma .................................. 52
3.3.8 Fungu 037: Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa Watumishi Serikalini -Tume ya Utumishi Serikalini ........................................................................ 53
3.3.9 Fungu 053: Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini - Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar ..................................... 53
3.3.10 Fungu 054: Programu ya Haki na Uwezeshaji Kishariah - Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana .......................... 54
3.3.11 Fungu 113: Programu ya Usimamizi wa Maadili ya Viongozi - Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ......................... 54

**SEHEMU YA NNE ........................................................... 56**
**4.0 SHUKRAN NA HITIMISHO ............................................ 56**

4.1 Shukrani ............................................................................. 56
4.2 Hitimisho............................................................................. 58

## VIAMBATISHO

Kiambatisho Nambari 1a: Makusanyo ya Mapato Julai/Machi 2025/2026 na Makadirio ya Mwaka 2026/2027 ........................ 59

Kiambatisho Nambari 1b: Muhtasari wa Upatikanajiwa Fedha 2025/2026 ............................................................................. 60

Kiambatisho Nambari 1c: Upatikanaji wa Fedha zaMiradi ya Maendeleo kwa Kipindi cha Julai 2025 - Machi 2026 na Makadirio kwa Mwaka 2026/2027 ........................................................... 64

Kiambatisho Nambari 2: Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 .................................................................. 66

Kiambatisho Nambari 3: Watumishi Waliopata Mafunzoya Muda Mfupi na Mrefu Nje ya Nchi kwa Mwaka 2025/2026 .................. 69

Kiambatisho Nambari 4: Hali ya Mashauri kwa Kipindi cha Julai 2025 - Machi 2026 ............................................................... 65

Kiambatisho Nambari 5a: Watumishi Walioajiriwa Kuanzia Julai, 2025 Hadi kufikia Machi, 2026................................................. 76

Kiambatisho Nambari 5B: Shughuli za Tume ya Utumishi Serikalini kwa Kipindi cha Julai, 2025 Hadi Machi, 2026 ........... 78

# MCHORO WA MUUNDO WA OFISI YA RAIS, KATIBA SHERIA UTUMISHI NA UTAWALA BORA



## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, na kuidhinisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kwa Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora.

2. **Mheshimiwa Spika,** naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehma, kwa kutuwezesha kukutana leo hii tukiwa na afya njema pamoja na uwezo wa kuendelea kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi tukiwa katika hali ya amani na utulivu.

### 1.1 Salamu za Pongezi

3. **Mheshimiwa Spika,** napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uongozi wake makini tangu alipoanza kuiongoza Zanzibar katika Serikali ya Awamu ya Nane. Nampongeza kwa kusimamia kwa ufanisi utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya kipindi kilichopita na Ilani ya CCM ya Mwaka 2025-2030. Mafanikio yanayoonekana katika miundombinu, elimu, afya, uchumi wa buluu na sekta nyingine ni ushahidi wa dhamira yake ya kuleta mageuzi ya kiuchumi Zanzibar. Aidha, tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa jitihada zake za kudumisha amani, utulivu, mshikamano, umoja na upendo miongoni mwa wananchi. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aendelee kumpa afya njema, hekima na busara ili tuendelee kunufaika na uongozi wake.

4. **Mheshimiwa Spika,** nampongeza Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, kwa uongozi wake thabiti katika kuratibu na kusimamia shughuli za Serikali ndani ya Baraza lako Tukufu, pamoja na mchango wake mkubwa katika kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza Ilani ya CCM katika vipindi viwili vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Awamu ya Nane.

5. **Mheshimiwa Spika,** naomba nikupongeze wewe binafsi pamoja na Naibu Spika kwa kuliongoza Baraza hili Tukufu kwa umakini, weledi na ufanisi hadi kufikia maamuzi mbalimbali yenye tija kwa maendeleo ya Zanzibar. Aidha, napenda kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati mbalimbali za Baraza hili kwa kusimamia utekelezaji wa mipango ya Serikali na kuhakikisha matumizi sahihi ya fedha, madaraka na rasilimali mbalimbali za Serikali.

6. **Mheshimiwa Spika,** natoa shukurani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Machano Othman Said, Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Mfenesini, pamoja na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Azza Januari Joseph, kwa ushauri na miongozo wanayoendelea kuitoa tangu kuanzishwa kwa Kamati hii mpya. Tunawashukuru kwa michango yao muhimu na ushauri waliotupatia wakati wa ziara mbalimbali na katika maandalizi ya bajeti hii. Kamati hii ina wajumbe wenye weledi na uzoefu wa hali ya juu, na Wizara ina matarajio makubwa ya kuendelea kunufaika na taaluma na umahiri wao katika kuendeleza ajenda za maendeleo.

7. **Mheshimiwa Spika,** Nawashukuru kwa dhati wananchi wa Jimbo la Makunduchi kwa ushirikiano wao wa karibu na imani wanayoendelea kunipa katika kuwawakilisha katika Baraza lako Tukufu, pamoja na mshikamano wao katika kusukuma mbele juhudi za maendeleo ya Jimbo letu. Aidha, naishukuru familia yangu hususan mke wangu mpendwa na watoto wangu kwa upendo, uvumilivu na ushirikiano wao unaoniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi.

8. **Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa hiki ni miongoni mwa vikao vya kwanza vya bajeti baada ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2025, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kushika nafasi za juu za kuiongoza Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nafasi walizokabidhiwa ni uthibitisho wa imani kubwa waliyopewa na wananchi kuhusu

uwezo na dhamira yao ya kuendeleza mageuzi ya kiuchumi kwa manufaa ya Taifa letu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awawezeshe kutekeleza dhamira hiyo.

### 1.2 Mafanikio ya Wizara katika Mwaka wa Fedha 2025/2026

9. **Mheshimiwa Spika,** sote tunashuhudia maendeleo ya haraka yaliyopatikana Zanzibar katika sekta mbalimbali chini ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Nane. Mafanikio haya yanatokana na mwelekeo na maono ya Mheshimiwa Rais katika kuleta mageuzi ya kiuchumi na kijamii kwa manufaa ya wananchi wa Zanzibar.

10. **Mheshimiwa Spika,** napenda kwa muhtasari kuwasilisha mafanikio yaliyopatikana katika Sekta za Sheria, Utumishi na Utawala Bora katika Mwaka wa Fedha 2025/2026. Mafanikio haya yanaonesha hatua muhimu iliyofikiwa katika kuimarisha utendaji wa Serikali na yataendelea kuwa msingi wa kupanga na kutekeleza vipaumbele vya mwaka ujao.

***Sekta ya Sheria***

a) Uendelezaji na uimarishaji wa miundombinu ya Mahkama unaendelea kutekelezwa kupitia miradi ya ujenzi wa majengo ya Mahakama za Mikoa na Wilaya Unguja na Pemba. Hatua hii imechangia kwa kiasi kikubwa kusogeza huduma za mahkama karibu na wananchi na kuboresha upatikanaji wa haki. Sambamba na hilo, Mahakama imeandaa na kuhuisha kanuni na miongozo muhimu ikiwemo Kanuni za ushahidi kwa njia ya kielektroniki, usikilizaji na ufunguaji wa mashauri kwa njia ya kielektroniki, Kanuni za Madai Madogo na Kanuni za Ada za Mahkama;

b) Ofisi imefanikiwa kutekeleza kwa ufanisi Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia (Mama Samia Legal Aid Campaign) kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ikiwa ni sehemu ya jitihada za Serikali kusogeza huduma za haki karibu na wananchi. Kupitia kampeni hii, mikoa yote mitano na wilaya 11 za Unguja na Pemba zilifikiwa, na jumla ya wananchi 422,908 walipata huduma za msaada wa kisheria, wakiwemo wanawake 209,185 na wanaume 213,723.

Aidha, kampeni ilipokea migogoro 749 inayohusu masuala mbalimbali kama vile ardhi, mirathi, ndoa, ajira, udhalilishaji na ukatili wa kijinsia, matunzo ya watoto na masuala mengine ya kisheria, ambapo migogoro 259 ilitatuliwa papo kwa papo, hatua iliyochangia kuimarisha upatikanaji wa haki na kupunguza migogoro katika jamii. Migogoro 490, imewasilishwa katika Taasisi husika kwa utatuzi na Wananchi wameunganishwa na Watoa Msaada wa Kisheria katika maeneo yao ambao wanawasaidia kuwapa miongozo juu ya kufuatilia migogoro yao;

c) Juhudi kubwa zimefanywa kuimarisha mfumo wa kisheria wa kudhibiti utakatishaji wa fedha haramu kwa kufanya mapitio ya sheria mbalimbali zenye mnasaba na eneo hili. Hatua hii ina mchango mkubwa katika kuiwezesha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuendelea kuzingatia na kutekeleza kwa ufanisi masharti na viwango vya kimataifa katika mapambano dhidi ya utakatishaji wa fedha haramu;

d) Ofisi kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa kushirikiana na Taasisi husika ilifanikiwa kuandaa jumla ya kanuni 22. Aidha, matangazo ya kisheria 107 yameandaliwa na kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali;

e) Ofisi kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu iliendelea kuiwakilisha serikali kwenye mashauri ya kesi za madai na kutoa ushauri wa kisheria kuhusiana na mashauri hayo. Jumla ya kesi 19 zilifunguliwa mahkamani, kati ya hizo, kesi 16 zilisikilizwa na kumalizika ambapo serikali ilifanikiwa kushinda kesi 15 na kesi 1 imemalizika kwa njia ya makubaliano. Aidha, jumla ya Indhari 24 za kuishitaki serikali zilipokelewa na zinaendelea kufanyiwa kazi;

f) Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kupitia Kikosi Kazi cha Kupambana na Uhalifu Mkubwa wa Kupangwa na Unaovuka Mipaka imefanya jumla ya operesheni 28 ambazo zinahusisha makosa ya dawa za kulevya, usafirishaji haramu wa binadamu na usafirishaji haramu wa silaha za moto. Katika operesheni hizo jumla ya watuhumiwa 23 wamekamatwa na kufikishwa katika vyombo vya kisheria husika kwa ajili ya hatua stahiki;

g) Aidha, Kikosi Kazi kimepokea na kufanyia kazi jumla ya taarifa 6 za matukio ya kihalifu kutoka taasisi mbali mbali za upelelezi za Kimataifa. Vile vile, kwa kushirikiana na Kikosi Kazi cha Tanzania Bara imeweza kupambana na usafirishaji haramu unaohusisha Tanzania na kushirikiana na Kituo Jumuishi cha Kuchunguza Makosa ya Kiuchumi ambapo jumla ya kesi 4 zinazohusisha uhalifu wa kifedha zimewezakuchunguzwa. na

h) Wizara, kupitia Ofisi ya Mufti Mkuu na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, imeendelea kuwa kiungo muhimu katika kuimarisha amani, umoja na utulivu wa kijamii. Taasisi hizi zimeendelea kutoa huduma bora za ibada ya hijja, utoaji wa misaada, usambazaji wa zaka na sadaka kwa wananchi. Aidha, juhudi za Wizara kupitia Ofisi ya Mufti Mkuu zimekuwa na mchango mkubwa katika kuimarisha upendo, umoja na mshikamano miongoni mwa wananchi.

***Sekta ya Utumishi***

a) Ofisi imeendelea kutekeleza hatua za kimkakati za kuimarisha ufanisi na matumizi endelevu ya Mifumo ya Kielektroniki ya Utoaji Huduma katika Utumishi wa Umma kwa lengo la kukuza ubora wa huduma, kuongeza uwajibikaji na kushughulikia changamoto mbalimbali za kiutendaji zilizojitokeza baada ya kukamilika na kuanza kutumika kwa mifumo hiyo. Hatua hizo zimejumuisha utoaji wa msaada wa kiufundi, maboresho ya mifumo na ufuatiliaji wa matumizi ya mifumo, ikiwemo Mfumo wa Maombi ya Ajira (ZanAjira), Mfumo wa Taarifa za Watumishi na Malipo (HR-PayMIS) pamoja na Mfumo wa Huduma za Serikali (ZGSD);

b) Ofisi imeanza kutekeleza agizo la Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, la kuanzisha Mikataba ya Utendaji (Performance Contracts) kwa viongozi wa Wizara na taasisi mbalimbali za Serikali. Mfumo huu unalenga kuongeza uwajibikaji, uwazi na ufanisi katika utoaji wa huduma za umma, huku ukisaidia kufuatilia utekelezaji wa sera, miradi na malengo ya maendeleo. Hadi sasa, miongozo na zana za usimamizi wa utendaji zimeandaliwa kwa ajili ya utekelezaji katika Wizara na Taasisi za Serikali. Utekelezaji wa mikataba hii

utaimarisha utawala bora unaotilia mkazo matokeo, uwajibikaji na utoaji wa huduma bora kwa wananchi na unatarajiwa kuanza utekelezaji wake mwaka ujao wa fedha;

c) Wizara imefanikiwa kuchukua hatua za kisera na kiutendaji za kuimarisha maslahi ya watumishi wa umma, hususan katika maeneo ya mishahara na maposho, kwa lengo la kuongeza motisha, uwajibikaji na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali. Hatua hizo zimehusisha uimarishaji wa miundo na vigezo vya ulipaji wa maposho mbalimbali, ikiwemo kuanzishwa kwa Posho la Nauli kwa Watumishi wa Umma, pamoja na kupanua wigo wa ulipaji wa Posho la Wakuu wa Divisheni katika Wizara na Taasisi, posho ambalo hapo awali lilikuwa likilipwa kwa Idara za Mipango, Sera na Utafiti pamoja na Idara ya Uendeshaji na Utumishi tu;

d) Ofisi imeimarisha Matumizi ya Miundo ya Utumishi (Scheme of Service) ambapo hivi sasa inatumika kwa ufanisi katika kupandisha vyeo, madaraja na marekebisho ya mishahara kuanzia Mwezi Julai, 2022. Hatua hii imepelekea kuondoa malalamiko mengi yaliyokuwepo ya kutozingatiwa ipasavyo uzoefu kwa watumishi wakongwe;

e) Ofisi imefanikiwa kuidhinisha Miundo ya Wizara, Mashirika ya Umma na Taasisi zinazojitegemea. Hatua hii imewezesha kuwepo kwa mgawanyo mzuri wa divisheni na majukumu pamoja na kuongeza ufanisi na tija katika utendaji na utoaji wa huduma;

f) Ofisi imetoa elimu kwa umma kuhusu masuala muhimu ya uimarishaji wa utumishi wa umma kupitia vyombo vya habari, hususan kupitia Televisheni yetu pendwa ya Wizara tuliyoianzisha ambayo ni Utawala Bora Online Television (UBTV).

g) Ofisi kupitia Chuo cha Utawala wa Umma (IPA) imetoa mafunzo elekezi kwa viongozi wakuu 72, watumishi wapya 5,219 na mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 318, pamoja na mafunzo ya maandalizi ya kustaafu kwa watumishi 274 Unguja na Pemba. Aidha, jumla ya wanafunzi 1,720 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu, wakiwemo watumishi wa umma 344 (asilimia 20) pamoja

na wananchi wengine 1,376 wakiwemo wafanyakazi kutoka sekta binafsi.

***Sekta ya Utawala Bora***

a) Ofisi imefanikiwa katika kufanya ukaguzi wa njia za kisasa kwa kuzingatia vipaumbele vya Serikali. Ukaguzi wa Hesabu za Serikali wa miradi mikubwa ya kimkakati, ikiwa ni pamoja miradi ya ujenzi wa Miundombinu ya Barabara, Vituo vya Afya, Miundombinu ya Maji Safi na salama, Ujenzi wa Masoko pamoja na Vituo vya wajasiriamali;

## 1.3 Changamoto Zilizopo na Hatua Zinazoendelea Kuchukuliwa

11. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha utekelezaji, Ofisi inaendelea kukabiliana na changamoto kadhaa zinazohitaji hatua endelevu ili kuimarisha utoaji wa huduma, kuongeza ufanisi wa matumizi ya rasilimali na kuhakikisha upatikanaji wa haki na utawala bora kwa wananchi. Changamoto hizo ni pamoja na:-

    a) Kwanza, ongezeko la mashauri na mahitaji ya huduma za haki limeendelea kuweka shinikizo kwa taasisi za utoaji haki. Baadhi ya mashauri, hususan yanayohusu jinai, madai, udhalilishaji, dawa za kulevya na makosa ya kiuchumi, yanahitaji uchunguzi wa kitaalamu, ushahidi wa kisayansi, mashahidi na uratibu wa karibu baina ya taasisi za haki jinai. Ofisi inaendelea kuimarisha miundombinu ya Mahkama, matumizi ya mifumo ya kidijitali, mafunzo kwa watendaji wa sekta ya sheria na ushirikiano baina ya Mahkama, Mashtaka, Polisi na taasisi nyingine za uchunguzi ili luongeza ufanisi katika kufanyia kazi mashauri yanayopolekewa.

    b) Pili, mageuzi ya kidijitali katika utumishi, sheria, ukaguzi na utawala bora yameongeza mahitaji ya vifaa, miundombinu, usalama wa taarifa na uwezo wa watumishi. Mifumo kama Zan-Ajira, e-Office, HR-PayMIS, mifumo ya usimamizi wa mashauri na mifumo ya ukaguzi inahitaji uwekezaji endelevu katika vifaa, mtandao, usalama wa kimtandao na mafunzo. Ofisi itaendelea kuimarisha miundombinu ya TEHAMA,

kuboresha mifumo iliyopo na kuwajengea uwezo watumishi ili kuongeza ufanisi na usalama wa taarifa.

c) Tatu, uwezo wa rasilimali watu katika maeneo maalumu bado unahitaji kuimarishwa ili kuendana na mahitaji mapya ya kiutendaji. Maeneo kama uchunguzi wa makosa ya kiuchumi, rushwa na utakatishaji wa fedha haramu na usimamizi wa mikataba ya utendaji yanahitaji utaalamu mahsusi. Ofisi itaendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu na kujenga uwezo wa kitaasisi kupitia programu za ndani na ushirikiano na washirika wa maendeleo.

d) Nne, uelewa wa wananchi kuhusu huduma za msaada wa kisheria, mifumo ya kuripoti rushwa, maadili ya viongozi na matumizi ya huduma za kidijitali bado unahitaji kuimarishwa. Serikali itaendelea kutoa elimu kwa umma kupitia mikutano ya wananchi, vyombo vya habari, majukwaa ya kidijitali na ushirikiano na taasisi za kiraia ili kuhakikisha wananchi wanazitumia huduma zinazotolewa na Serikali kwa ufanisi.

e) Tano, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mipango, miradi na mikataba ya utendaji bado unahitaji kuimarishwa zaidi. Kutokana na kuongezeka kwa majukumu na mageuzi yanayoendelea, Ofisi itaendelea kuimarisha mifumo ya ukusanyaji takwimu, ufuatiliaji wa matokeo na utoaji wa taarifa za utekelezaji ili kuhakikisha mipango na bajeti zinajikita katika matokeo yanayopimika.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

12. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Ofisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imesimamia mafungu ya bajeti 11 yaliyotekelezwa kupitia Programu kuu 14 ambazo zinatekelezwa na Idara na Taasisi zinazojitegemea zilizo chini ya Ofisi. Utekelezaji wa bajeti wa kila Programu umefanyika kama ifuatavyo: -

### 2.1 Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

13. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Ofisi kupitia Taasisi zilizo chini yake ilikadiriwa kukusanya mapato ya **Sh.2,414,369,160** ukilinganisha na **Sh.2,270,892,852** zilizokadiriwa mwaka 2024/2025, sawa na ongezeko la **Sh.143,476,308** (asilimia 6 ya ongezeko).

14. **Mheshimiwa Spika,** hadi Machi 2026, jumla ya Sh.747,096,289 zimekusanywa sawa na asilimia 31 ya makadirio. Makusanyo haya yanatokana na vyanzo mbalimbali kama inavyoonekana katika (Kiambatisho Nambari 1a).

### 2.2 Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

15. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Ofisi ilipangiwa kutumia jumla ya **Sh.131,337,472,653**. Kati ya fedha hizo, **Sh.49,385,547,320** zilipangwa kwa ajili ya mishahara, **Sh.25,915,252,800** kwa matumizi mengineyo, Sh.220,000,000 ikiwa ruzuku ya matumizi mengineyo kutoka kwa wahisani, **Sh.15,100,000,000** kwa Miradi ya Maendeleo inayofadhiliwa na SMZ, na **Sh.40,716,672,533** kwa Miradi ya Maendeleo inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo.

16. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2026, jumla ya **Sh.75,858,983,258** zimepatikana, sawa na asilimia 58 ya lengo. Kati ya fedha hizo, **Sh.46,142,633,400** zilitumika kwa shughuli za kawaida, mishahara na ruzuku; **Sh.8,696,815,982** zilitumika katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo inayofadhiliwa na SMZ;

**Sh.20,898,140,876** zilipatikana kwa Miradi inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo; na **Sh.121,393,000** zilipatikana ikiwa ni ruzuku kutoka kwa wahisani (Kiambatisho Nambari 1b na 1c).

### 2.3 Vipaumbele vya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**17. Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 OR-KSUUB ilitekeleza Mpango na Bajeti kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo: -

i. Kuendeleza matumizi ya Mifumo ya Kielektroniki katika Utumishi wa Umma;
ii. Kukamilisha na kuendeleza Miradi Mikubwa ya Ujenzi wa Miundombinu ya Mahkama
iii. Kuanzisha programu za mafunzo ya kujenga umahiri wa Watumishi wa Umma;
iv. Kuratibu na kusimamia masuala ya dini pamoja na mali za amana;
v. Kuendelea kuimarisha utendaji katika taasisi za Sheria na kufanya marekebisho ya Sheria mbalimbali;
vi. Kuendelea kuongeza uwelewa kwa jamii juu ya masuala ya msaada wa kisheria; na
vii. Kusimamia misingi ya utawala bora, maadili na kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa, pamoja na ukaguzi na udhibiti wa rasilimali za umma.

### 2.4 Malengo Makuu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**18. Mheshimiwa Spika,** ili kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele vya Ofisi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imepanga kutekeleza malengo yafuatayo: -

i. Kuimarisha upatikanaji wa haki na utawala wa sheria;
ii. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo ya Watumishi wa Umma kwa ajili ya upatikanaji wa Rasilimali Watu wenye sifa;
iii. Kusimamia na kuratibu Programu ya Utekelezaji wa Mpango wa Mabadiliko ya Utumishi wa Umma PSRP II;

iv. Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika shughuli na utoaji wa huduma za Serikali na kukuza uchumi;
v. Kuimarisha misingi ya Utawala Bora, Uwajibikaji na maadili katika utendaji wa shughuli za Serikali pamoja na kuimarisha umoja na mshikamano; na
vi. Kuimarisha usimamizi wa udhibiti na rasilimali za Serikali na kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu uchumi.

## 2.5 Utekelezaji wa Malengo ya Ofisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**19. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Ofisi imetekeleza malengo yake kupitia mafungu ya bajeti 11 na Programu Kuu 14. Malengo ya utekelezaji kwa kila Fungu la Bajeti na Programu kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ni kama inavyowasilishwa hapo chini.

**20. Mheshimiwa Spika,** kati ya Programu hizi, Programu kuu nne (4) za fungu G01 zinasimamiwa na kutekelezwa kupitia Idara zilizo chini ya Katibu Mkuu na Programu Kuu 10 zinatekelezwa na Taasisi zinazojitegemea.

**21. Mheshimiwa Spika,** Ofisi katika utekelezaji wa malengo iliyojipangiwa kupitia Programu zilizo chini yake, Ofisi ilizingatia usawa wa kijinsia kwa lengo la kuendeleza azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kujenga mfumo wa haki na kutoa fursa sawa kwa wananchi wote kwa kuzingatia usawa wa kijinsia.

## 2.6 Utekelezaji kwa Kuzingatia Usawa wa Kijinsia

**22. Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia usawa wa kijinsia, kupitia Idara ya Mipango ya Rasilimali Watu na Maendeleo ya Watumishi, ambayo inasimamia maendeleo ya rasilimali watu kwa Serikali, Ofisi imeendelea kuratibu fursa za masomo kwa kuzingatia misingi ya usawa na haki. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 jumla ya watumishi 1,519 walipata fursa za masomo katika ngazi mbalimbali na asilimia 59 ya nafasi hizo walipatia watumishi wa umma wanawake. Kwa upande wa ajira, katika kipindi cha Julai

2025 hadi Machi 2026, Serikali iliajiri jumla ya watumishi 772 Unguja na Pemba ambapo wanaume 316 na wanawake 456.

**23. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Mahakama, jumla ya Sh. 818,000,000 sawa na asilimia 2 ya bajeti ya Mahakama zilitengwa kwa ajili ya shughuli za kuimarisha usawa wa kijinsia. Fedha hizi zimeelekezwa katika maandalizi ya miongozo ya utekelezaji, utoaji wa mafunzo, pamoja na ushiriki katika majukwaa ya kikanda yanayohusu masuala ya kijinsia. Miongoni mwa miongozo iliyoandaliwa ni Mpango Mkakati wa Kijinsia unaojumuisha shughuli zote za Mahkama sambamba na mifumo ya ufuatiliaji na tathmini ili kuhakikisha utekelezaji wenye tija.

**24. Mheshimiwa Spika,** mahkama pia imeweka miundombinu rafiki kama vile vyumba vya dharura na vya kunyonyeshea watoto katika majengo mapya ya Mahkama, kwa lengo la kuhakikisha mazingira ya Mahkama yanakuwa jumuishi kwa watumishi na watumiaji wa huduma za upatikanaji wa haki. Juhudi hizi zinalenga kuhakikisha uwiano wa fursa kwa watumishi, utoaji wa stahiki na maslahi bila ubaguzi wa kijinsia, pamoja na uwekaji wa mazingira rafiki ya kazi yanayozingatia mahitaji maalum ya wanawake, wanaume na makundi yote. Hatua hizi zimeendelea kuongeza tija na motisha kwa watumishi na kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi katika ngazi zote za Mahkama Unguja na Pemba.

**25. Mheshimiwa Spika,** Ofisi kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la UN Women imeendelea kutekeleza Mradi wa Utoaji wa Haki kwa Kuzingatia Jinsia, unaolenga kuwasaidia wanawake, katika kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia. Kwa Mwaka Fedha 2025/2026 wananchi 13,364 walinufaika na huduma zilizotolewa kati yao wanawake walikuwa 8,008(60%) na wanaume 5,356. Hali hii inaonesha kuongezeka kwa mwitikio wa wanawake katika kupata huduma za haki na imani yao kwa mifumo ya utoaji haki.

**26. Mheshimiwa Spika,** katika kuzingatia usawa wa kijinsia na ustawi wa watoto, Ofisi imeendelea kushughulikia maeneo mbalimbali yenye mchango mkubwa katika kuimarisha haki, ustawi wa jamii pamoja na amani na utulivu nchini. Kupitia Ofisi

ya Mufti Mkuu, migogoro 543 ya ndoa, migogoro 640 ya talaka na migogoro 158 inayohusu malezi ya watoto, mirathi, pamoja na kutelekezwa imetatuliwa na wanawake wamekuwa wanufaika wakubwa kutokana na utatuzi uliopatikana.

27. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio haya, bado zipo changamoto zinazohitaji kushughulikiwa ili kuimarisha zaidi utekelezaji wa bajeti kijinsia. Changamoto hizo ni pamoja na uelewa mdogo wa baadhi ya watendaji kuhusu dhana ya bajeti kijinsia, Ofisi itaendelea kutoa mafunzo kwa Taasisi zilizo chini yake ili kuhakikisha utekelezaji wa kazi zinazopangwa unazingatia usawa wa kijinsia, sambamba na kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini ili kuhakikisha utekelezaji wake unakuwa endelevu na wenye matokeo yenye tija na maslahi mapana kwa jamii.

## 2.7 Utekelezaji wa Bajeti kwa Mafungu na Programu

### 2.7.1 Fungu G01: Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora

28. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora inasimamia Programu nne (4) na Taasisi mbili za ruzuku ambazo ni: -

**i Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Sheria**

29. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ipo chini ya Idara ya Katiba na Msaada wa Kisheria kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 imetekeleza yafuatayo:

   i. Idara imetoa elimu kuhusu masuala ya msaada wa kisheria kwa wananchi mbalimbali kupitia maonesho ya Siku ya Sheria Zanzibar yaliyofanyika Pemba kuanzia tarehe 3 hadi 8 Februari 2026. Aidha, jumla ya wananchi 576 walipewa huduma za msaada wa kisheria, wakiwemo wanajamii 176 (wanawake 77 na wanaume 102), wanafunzi 373 (wanaume 155 na wanawake 218) pamoja na viongozi 24;

   ii. Idara, kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), imetoa elimu ya msaada wa kisheria kupitia

mikutano ya wazi Unguja na Pemba ambapo jumla ya wananchi 1,572 (wanawake 1,058 na wanaume 514) walifikiwa;

iii. Jumla ya taasisi 5 za watoaji msaada wa kisheria, jumuiya za wasaidizi wa sheria 14 na Vituo vya msaada wa kisheria 2 vimekaguliwa na kubaini changamoto mbalimbali zinazowakabili katika utoaji wa huduma na kisheria na kuzipatia ufumbuzi;

iv. Mafunzo ya kuwajengea uwezo yametolewa kwa wanafunzi wapya waliojiunga na vituo vya msaada wa kisheria vya Zanzibar University Legal Aid Clinic na Zanzibar Law Resource Centre Legal Aid Clinic kuhusu maadili ya utoaji wa huduma za kisheria, ambapo jumla ya wanafunzi 40 walishiriki (wanawake 18 na wanaume 22); na

v. Idara, kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, iliandaa kikao kazi kujadili Mpango Kazi wa Kitaifa wa Haki za Binadamu na Biashara. Aidha, Idara imeshiriki na kuwasilisha maoni ya Tanzania kuhusu Rasimu ya Mswada wa Sheria ya Kutokomeza Ukeketaji wa Wanawake na Wasichana, na maoni hayo yalipokelewa na kukubaliwa.

vi. Kwa upande wa Matumizi ya Ruzuku kutoka kwa Wahisani wa Maendeleo, shughuli zifuatazo zimetekelezwa; -

a) Maafisa wa Dawati la Jinsia na Ulinzi wa Mtoto wamepatiwa mafunzo kuhusu usimamizi wa kesi za ulinzi wa Mtoto kupitia Muongozo wa Mafunzo ya Polisi. Jumla ya Maafisa110 wamepatiwa mafunzo kati ya hao, Maafisa 84 kutoka Unguja (Wanaume 49 na Wanawake 36) na Maafisa 25 kutoka Pemba (Wanaume 8 na Wanawake 17);

b) Maafisa 40 walipatiwa mafunzo kuhusu Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Ulinzi wa Mtoto; kati yao, maafisa 15 (wanaume 5 na wanawake 10) walitoka Pemba na maafisa 25 (wanaume 15 na wanawake 10) walitoka Unguja; na

c) Mapitio ya Mpango Mkakati wa Haki kwa Mtoto yamefanyika ambapo mshauri elekezi amewasilisha Ripoti ya Awali (Inception Report) inayoainisha mbinu na mpango kazi wa kuandaa mkakati mpya wa marekebisho ya mfumo wa haki kwa watoto na wanawake kwa Mwaka 2026/2030.

30. **Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa Fedha 2025/2026 Programu hii ilipangiwa **Sh.348,975,000** (mishahara **Sh.126,183,000** na matumizi mengineyo **Sh.222,792,000**). Hadi kufikia Machi 2026, **Sh.178,103,245** (sawa na asilimia 51 ya lengo) zimepatikana ambapo **Sh.154,748,714** zilitumika kwa mishahara (sawa na asilimia 123 ya lengo) na **Sh.23,354,531** (sawa na asilimia 10 ya lengo) zilitumika kwa matumizi mengineyo. Aidha, Ruzuku kutoka kwa Wahisani wa Maendeleo **Sh.85,000,000** zilipangwa. Hadi kufikia Machi, 2026 **Sh.95,023,000** zilipatikana (sawa na asilimia 112 ya lengo) (**Kiambatisho Nambari 1b)**

**ii Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora**

31. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Idara ya Utawala Bora. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, kazi zifuatazo zilitekelezwa:

   i. Tathmini ya utekelezaji wa Mikataba ya Utendaji Kazi ilifanyika, ambapo Idara kwa kushirikiana na Mshauri Elekezi ilitoa mafunzo kwa Wizara saba ikiwemo Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora ili kuimarisha uelewa na uwezo wa uandaaji na usimamizi wa mikataba hiyo;
   ii. Idara ilitayarisha na kurusha hewani vipindi 31 vya habari na vipindi 26 vya matukio ya Serikali kupitia Televisheni Mtandao ya Utawala Bora (UBTV);
   iii. Idara ilishiriki Mkutano wa 110 wa TBC wa Elimu kwa Umma uliofanyika Arushwa (23–27 Machi 2026), na kuandaa dokumentari za Maadili na Haki za Binadamu, Wiki ya Utumishi wa Umma, pamoja na Maadhimisho ya Biashara yaliyofanyika Nyamanzi; na
   iv. Mpango wa kutathmini Taasisi za Umma kwa kuzingatia vigezo vya Utawala Bora umetayarishwa ili kuhuishwa na kuendana na mahitaji ya sasa.

32. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Programu hii ilipangiwa **Sh.327,263,000** (mishahara **Sh.125,342,000** na **Sh.201,921,000** matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi 2026, **Sh.151,578,601** zimepatikana (sawa na asilimia 46 ya lengo)

ambapo **Sh.129,213,176** zilitumika kwa mishahara (sawa na asilimia 103 ya lengo) na **Sh.22,365,425** zilitumika kwa matumzi mengineyo (sawa na asilimia 11 ya lengo) **(Kiambatisho Nambari 1b).**

**iii Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora**

**33. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Idara ya Utumishi na Uendeshaji na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. -

**34. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Idara ya Utumishi na Uendeshaji, kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 kazi zifuatazo zimetekelezwa:

i. Idara imeendelea kusimamia masuala ya kiutumishi kwa kutoa likizo, posho na mafunzo; watumishi 28 walipatiwa likizo (25 kawaida, 3 uzazi), 30 walilipwa posho mbalimbali, 33 walifanyiwa tathmini ya utendaji kazi, na 9 walipandishwa daraja; na

ii. Utoaji wa taarifa umeimarishwa kupitia redio, televisheni, magazeti, tovuti ya Wizara na mitandao ya kijamii, ukieleza mafanikio ya Utumishi wa Umma chini ya uongozi wa Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi.

**35. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Idara ilipangiwa kutumia **Sh.3,633,619,000** (mishahara **Sh.2,006,647,000** na matumizi mengineyo Sh.1,626,972,000). Hadi kufikia Machi 2026, **Sh.2,208,658,174** zilipatikana (sawa na asilimia 61 ya lengo) kati ya hizo **Sh.1,313,606,556** zilitumika kwa mishahara (sawa na asilimia 65 ya lengo) na **Sh.895,051,618** zilitumika kwa matumizi ya kawaida (sawa na asilimia 55 ya lengo) **(Kiambatisho Nambari 1b).**

**36. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, kazi zifuatazo zimetekelezwa:-

i. Kuratibu na kusimamia mapitio ya Sera ya Msaada wa Kisheria na Sheria ya Majukumu ya Kijamii. Aidha, Idara imeratibu na kuandaa nyaraka za kisera na kisheria na kuziwasilisha katika Kamati ya Makatibu Wakuu na Kamati ya Baraza la Mapinduzi;

ii. Kuandaa na kuratibu utekelezaji wa Mipango ya bajeti, ripoti za robo, nusu na mwaka kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na kuandaa mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 na kuziwasilisha nyaraka zinazohusiana na kazi hizo kwa mamlaka husika;

iii. Kuendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za programu na miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Ofisi kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo. Aidha, maandalizi ya Mradi wa Mageuzi katika Utumishi wa Umma yamefanyika kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Benki ya Dunia (TRANSFORM).

37. **Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Idara ilipangiwa **Sh.412,782,500** (**Sh.255,053,000** mishahara na **Sh.157,729,500** matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi 2026, **Sh.211,306,033** zimepatikana (sawa na asilimia 51 ya lengo), ambapo **Sh.143,593,637** ni mishahara (sawa na asilimia 56 ya lengo) na **Sh.67,712,396** zimetumika kwa matumizi mengineyo (sawa na asilimia 43 ya lengo) **(Kiambatisho Nambari 1b)**.

**Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

38. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, kwa kushirikiana na Taasisi zilizo chini ya Ofisi, imeratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi mitatu ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama ifuatavyo:-

***a) Mradi wa Uwezeshaji na Upatikanaji wa Haki Kisheria Awamu ya Pili (LEAP II)***

39. **Mheshimiwa Spika,** Mradi unatekelezwa kupitia Skuli ya Sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Chuo cha Mafunzo na Idara ya Katiba na Msaada wa Kisheria. Mradi umejikita katika kujenga uwezo wa Sekta ya Sheria na kuimarisha upatikanaji wa haki kwa wananchi. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Mradi ulitumia **Sh.1,004,746,625** sawa na asilimia 82 ya lengo, na kazi zilizotekelezwa ni:

i Skuli ya Sheria imetayarisha Mfumo wa Kujifundishia 'E-learning' kwa Maafisa Sheria ambao utawezesha kujifunza popote bila ya kuhudhuria darasani. Mfumo huo umezinduliwa tarehe 23 Januari 2026;

ii Maafisa Sheria 350 wamejengewa uwezo kwa kupatiwa mafunzo ya Uandishi wa Hukumu, Mashtaka, Uchunguzi na Matunzo Unguja na Pemba;

iii Elimu ya msaada wa kisheria kupitia mikutano ya wazi Unguja na Pemba imetolewa. Jumla ya wananchi 1,572 walipatiwa uelewa kuhusu haki za binadamu, ambapo wanawake ni 1,058 na wanaume ni 514;

iv Idara ya Katiba na Sheria, kwa kushirikiana na Shirika la UNDP, iliandaa mafunzo ya siku mbili kuhusu Akili Mnemba (AI) kwa watoa msaada wa kisheria. Lengo la mafunzo hayo ni kuhamasisha matumizi ya Akili Mnemba (AI) katika masuala ya upatikanaji wa haki. Jumla ya watoa huduma ya msaada wa kisheria 51 (wanawake 14 na wanaume 37) walipatiwa mafunzo hayo.

***b) Mradi wa Utoaji wa Haki kwa Kuzingatia Jinsia ili Kuwasaidia Wanawake Kukabiliana na Kesi za Udhalilishaji na Ukatili wa Kijinsia Zanzibar (UN WOMEN)***

**40. Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unatekelezwa na Mahkama Kuu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Idara ya Katiba na Msaada wa Kisheria. Mradi umejikita katika kuwajengea uwezo wanawake ili kukabiliana na kesi za udhalilishaji na ukatili wa kijinsia. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, **Sh.100,000,000** zimetumika, sawa na asilimia 70 ya lengo, katika kazi zifuatazo:-

i Idara kwa kushirikiana na Shirika la UN Women ilizindua pamoja na kutoa Mafunzo ya siku mbili ya mwongozo wa uanzishwaji na Uratibu wa Jukwaa la Taifa la Haki za Wanawake na Wasichana 2025 ambapo jumla ya washiriki 51 waliopatiwa mafunzo, kati ya hao, Wanawake 37 na wanaume 14;

ii Muongozo wa Utoaji Hukumu (Sentencing Guideline) umetayarishwa na kutafsiriwa kwa lugha nyepesi ili kurahisisha utendaji kazi kwa maafisa wa mahkama na wahusika wengine katika sekta ya haki;

iii Mafunzo yalitolewa ili kuongeza uwezo kwa watumishi wa Kitengo cha Ulinzi wa Mashahidi na Wahanga (Victims and Witness Protection Unit) cha Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ili kuwasaidia mashahidi na waathiriwa wa matukio ya udhalilishaji na ukatili wa kijinsia (SGBV).

***c) Mradi wa Kujenga Mfumo Endelevu wa Kupambana na Rushwa Tanzania (BSAAT).***

**41. Mheshimiwa Spika,** Mradi huu ni wa miezi 15 na utekelezaji wake unazihusisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mahkama Kuu Zanzibar, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Mrajis wa Taasisi Zisizo za Kiserikali, Wakala wa Usajili wa Mali na Biashara, Jeshi la Polisi, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora na Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, jumla ya **Sh.2,160,000,000** zilitumika, sawa na asilimia 50 ya lengo, na kazi zilizotekelezwa ni:-

a) Kuanzishwa na kuimarishwa mifumo ya kidijitali ya usimamizi wa kesi na taarifa kwa taasisi ya (ZAECA na OCAG), jambo lililoongeza uwazi, ufanisi na uwezo wa kufuatilia mwenendo wa kesi;

b) Kuimarisha ufanisi kwa taasisi za haki jinai katika kubadilishana taarifa kwa wakati na kwa ufanisi zaidi; na

c) Kutoa mafunzo maalum kwa wachunguzi, waendesha mashtaka, Waheshimiwa Mahakimu na Majaji, pamoja na watumishi wa Mahkama na taasisi za usimamizi wa kifedha.

**Ofisi Kuu Pemba**

42. **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 kazi zifuatazo zimetekelezwa: -

i. Ofisi ilisimamia uratibu wa majukumu ya Ofisi kwa upande wa Pemba, ambapo imeendelea kufanya vikao kazi kwa kuzitembelea Taasisi za SMZ. Lengo ni kuendelea kusimamia utumishi uliotukuka kwa kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo. Miongoni mwa Taasisi zilizotembelewa ni Kamisheni ya Ardhi, ZEMA, Wakala wa Karakana Kuu ya Magari, Shirika la Nyumba, pamoja na Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda; na

ii. Vikao 5 vimeratibiwa vikihusisha kada mbalimbali za watumishi pamoja na wakuu wa taasisi za OR/KSUUB Pemba, kwa lengo la kujadili mafunzo, haki na wajibu wa watumishi. Aidha kikao maalum kiliandaliwa kwa maafisa usafirishaji kuhusu uelewa na uzingatiaji wa sheria, kanuni na miongozo ya utumishi.

43. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Ofisi Kuu Pemba imepangiwa kutumia **Sh.732,248,000**. (**Sh.482,248,000** mishahara na **Sh.250,000,000** matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi 2026, fedha zilizopatikana ni S**h.371,544,700** (sawa na asilimia 51 ya lengo) ambapo **Sh.295,744,700** ni mishahara (sawa na asilimia 61 ya lengo) na **Sh.75,800,000** zimetumika kwa matumizi mengineyo (sawa na asilimia 30 ya lengo) **(Kiambatisho Nambari 1b).**

**iv Programu ya Usimamizi na Uendelezaji wa Watumishi wa Umma**

44. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Idara ya Mipango ya Rasilimali Watu na Maendeleo ya Watumishi pamoja na Idara ya Miundo ya Taasisi na Maslahi ya Watumishi.

45. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Idara ya Mipango ya Rasilimali Watu na Maendeleo ya Watumishi, katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 kazi zifuatazo zimetekelezwa:-

i. Idara imeratibu mafunzo yanayotolewa na Wahisani wa Maendeleo, ambapo jumla ya watumishi 25 (wanaume 17 na wanawake 8) wamehudhuria mafunzo mafupi nchini India; watumishi 3, wote wanaume, wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu; watumishi 4, wote wanawake, wamehudhuria mafunzo mafupi nchini Japan; watumishi 5, wote wanaume, wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu nchini Korea; na mtumishi 1, mwanaume, amehudhuria mafunzo ya muda mrefu nchini China;

ii. Idara, kwa kushirikiana na Chuo cha Utawala wa Umma, imetoa mafunzo ya kuwajengea uwezo Viongozi na Watendaji Wakuu wa Wizara na Taasisi zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mafunzo hayo yalilenga kuhakikisha kuwa viongozi hao wanatekeleza majukumu yao wakiwa na uelewa mpana wa mwelekeo wa Serikali na uwezo wa kuziongoza Taasisi na Idara kwa weledi, ufanisi na tija;

iii. Idara, kwa kushirikiana na wataalamu wa TEHAMA kutoka Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (SMT), inaendelea kuandaa Mfumo wa Mahitaji ya Watumishi (ZHRAIS) ambapo hivi sasa umekamilika kwa asilimia 85 na unatarajiwa kuanza kutumika Julai 2026. Mfumo huo utawezesha kubaini mahitaji sahihi ya watumishi katika Wizara, Idara na Vitengo. Aidha, mfumo wa HR-PayMIS umeunganishwa na Platinum Credit Zanzibar Limited kwa lengo kurahisisha na kuboresha utaratibu wa malipo ya mikato kwa watumishi waliokopa; na

iv. Idara imeratibu utoaji wa ajira kwa Wizara na Taasisi mbalimbali za SMZ ambapo jumla ya vibali 31 vya ajira vimetolewa. Aidha, Idara imekamilisha maridhiano ya uhamisho katika Wizara na Taasisi mbalimbali za SMZ ambapo jumla ya maridhiano 281 yamekamilishwa.

46. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu kwa upande wa Idara ya Mipango Rasilimali Watu na Maendeleo ya Watumishi ilipangiwa kutumia **Sh.1,309,843,420**

(**Sh.461,471,120** mishahara na **Sh.848,372,300** matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi 2026, **Sh.958,326,853** zimepatikana (sawa na asilimia 73 ya lengo) ambapo **Sh.484,920,575** zimetumika kwa mishahara (sawa na asilimia 105 ya lengo) na **Sh.473,406,278** zimetumika kwa matumizi mengineyo (sawa na asilimia 56 ya lengo) **(Kiambatisho Nambari 1b)**.

**47. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi. Kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 kazi zifuatazo zilitekelezwa:

i. Idara imetayarisha Muongozo wa Usimamizi wa Mikataba ya Utendaji Kazi (Performance Contract Guidelines) pamoja na 'Legal Notice' kwa lengo la kuweka misingi madhubuti ya utekelezaji wenye ufanisi na uwajibikaji;

ii. Kuandaa Muongozo wa Uandaaji wa Mkataba wa Utoaji Huduma kwa Umma. Aidha, mafunzo ya kuwajengea uwezo yametolewa kwa Watendaji wa taasisi tisa (9) za Umma za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar juu ya uandaaji na utekelezaji wa mkataba huo kwa mujibu wa mwongozo uliopo;

iii. Uhakiki umefanyika wa taarifa za watumishi kupitia Mfumo wa Taarifa za Watumishi na Malipo (HR-PayMIS) kwa Wizara 18 na Taasisi zinazozisimamia za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa upande wa Pemba ili kuhakikisha usahihi wa taarifa za watumishi. Aidha, mafunzo ya kuwajengea uwezo kuhusu matumizi sahihi ya mfumo yametolewa kwa viongozi na maafisa kwa upande wa Unguja na Pemba;

iv. Idara imekamilisha zoezi la uunganishaji wa mifumo (integration) kati ya Mfumo wa Taarifa za Watumishi na Malipo (HR-PayMIS), Mfumo wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) na Mfumo wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu Zanzibar (ZHESLB) ili kurahisisha utaratibu wa makato ya kila mwezi kwa watumishi wa umma;

v. Idara imeendelea kufanya marekebisho ya mshahara na stahiki nyengine za Watumishi ambapo jumla ya Watumishi 2,047 waliostahiki kufanyiwa marekebisho mbalimbali

walirekebishiwa na jumla ya Sh. 1,898,558,920 zimetumika kufanya marekebisho hayo;

vi. Idara imefanya mapitio na kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu miundo 15 ya kitaasisi na miundo mitano (5) ya kiutumishi katika Taasisi mbalimbali za Umma;

vii. Malalamiko 60 ya Watumishi yameshughulikiwa na kupatiwa ufumbuzi, kati ya hayo, 35 yanayohusu madai ya stahiki na 25 yanayohusu mafao ya kustaafu kazi. Aidha, mwongozo umetolewa wa kurejeshwa kazini kwa watumishi 12 waliosimamishwa kazi wakati wa kuazishwa Vyama vingi vya Siasa Mwaka 1992; na

viii. Miongozo na Matoleo 15 ya kiutumishi imetolewa ili kufafanua masuala mbalimbali ya kiutumishi na kurahisisha utekelezaji wa majukumu katika Taasisi za Serikali, Mamlaka, Mashirika na Taasisi zinazojitegemea.

**48. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu kwa upande wa Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi imepangiwa kutumia **Sh.894,569,200** (**Sh.684,569,200** mishahara na **Sh.210,000,000** matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi 2026, **Sh.701,314,892** zimepatikana (sawa na asilimia 78 ya lengo) ambapo **Sh.641,927,676** zimetumika kwa mishahara (sawa na asilimia 94 ya lengo) na **Sh.59,387,216** zimetumika kwa matumizi mengineyo (sawa na asilimia 28 ya lengo) **(Kiambatisho Nambari 1b).**

***Taasisi Zinazopokea Ruzuku***

**49. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Ofisi imeendelea kusimamia Taasisi mbili zinazopokea ruzuku ya mishahara na matumizi mengineyo. Taasisi hizo ni Chuo cha Utawala wa Umma na Skuli ya Sheria, ambapo hadi Machi 2026 Taasisi hizi zimetekeleza shughuli zifuatazo: -

**a) Chuo cha Utawala wa Umma (IPA)**

**50. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Chuo cha Utawala wa Umma kimetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Mafunzo Elekezi yametolewa kwa watumishi wapya 2,374 kati ya hao watumishi 476 ni kutoka Unguja na watumishi 1,898 kutoka Pemba;
ii. Chuo kimetoa mafunzo kwa viongozi mbali mbali wakiwemo Mawaziri, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu, Manaibu Makatibu na Wakuu wa Taasisi 187 kutoka katika wizara naTaasisi mbalimbali za Serikali. Miongoni mwa mada zilizowasilishwa ni: Sifa za Uongozi bora, Itifaki kwa viongozi, Uongozi wa Kimkakati, Majukumu, Usalama, Uadilifu na usiri katika Serikali, Maslahi ya Taifa, Utatuzi wa migogoro na Maadili katika Utumishi wa Umma;
iii. Mafunzo ya kujenga uwezo yametolewa kwa watumishi 180 wa Umma, yakihusisha mada mbalimbali zikiwemo uwekaji na usimamizi wa nyaraka za ofisi, huduma kwa mteja, itifaki na ustaarabu, pamoja na kanuni za Utumishi wa Umma. Mafunzo hayo yametolewa kwa watumishi wa ZIC Takaful, Kampuni ya Mwani, Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji, na Baraza la Mji Wilaya Kati Unguja;
iv. Jumla ya watumishi wanaotarajiwa kustaafu 42 wamepatiwa mafunzo;
v. Jumla ya wanafunzi 1,912 wamepatiwa mafunzo. Kati ya hao, 574 ni watumishi wa Serikali na 1,338 ni wananchi wengine; na
vi. Chuo kimewapa fursa ya mafunzo ya muda mrefu watumishi 5 katika kada na fani mbalimbali na kimewajengea uwezo wa kitaalamu watumishi wake 18 juu ya uandishi wa kumbukumbu za kikao, mifumo ya rasilimali watu na masuala ya uhasibu.

51. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Chuo kilipangiwa ruzuku ya **Sh.3,203,290,000** kwa malipo ya mishahara. Hadi kufikia Machi 2026, **Sh.2,498,273,043** zimepatikana (sawa na asilimia 78 ya lengo).

### b) Skuli ya Sheria Zanzibar

52. **Mheshimiwa Spika,** Skuli ya Sheria Zanzibar kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ilitekeleza kazi zifuatazo:

i. Jumla ya waombaji 107 walikidhi vigezo na kuchaguliwa kujiunga na Skuli ya Sheria kwa mwaka 2026, ulioanzia Januari, 2026;
ii. Skuli ya Sheria imekamilisha Kanuni za Mitihani (Examination Regulations). Kanuni hizo zitatoa mwongozo kwa wakufunzi wa Skuli kuhusu utungaji, ufanyaji, usimamizi na usahihishaji wa mitihani ya Skuli ya Sheria;
iii. Mafunzo ya Vitendo (Field Attachments) kwa wanafunzi 22 yamefanyika katika Kundi la Nne kuanzia tarehe 25 Agosti, 2025 na kumalizika tarehe 5 Januari, 2026. Mafunzo yamefanyika kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za Sheria za Zanzibar zikiwemo Afisa ya Mwanasheria Mkuu, Mahkama Kuu, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka – DPP, Afisi za Mawakili wa Kujitegemea pamoja na taasisi za Sheria za Tanzania Bara; na
iv. Wanafunzi 22 wamefanya mtihani wa kundi la nne (4) kuanzia tarehe 13 Januari 2026 hadi tarehe 27 Januari 2026. Aidha, mitihani ya uandishi (Written Practical Examinations - WPE) imefanyika kwa wanafunzi 16 wa kundi la tano (5) kuanzia tarehe 2 Februari 2026 hadi tarehe 11 Februari 2026 kwa mwaka wa masomo 2025/2026.

53. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Skuli ya Sheria ilipangiwa kutumia ruzuku ya Sh.**1,302,210,000**. (**Sh.679,810,000** mishahara na **Sh.622,400,000** matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi 2026, **Sh.759,175,549** zimepatikana (sawa na asilimia 58 ya lengo) ambapo **Sh.537,936,303** zimetumika kwa mishahara (sawa na asilimia 79 ya lengo) na **Sh.221,239,246** zimetumika kwa matumizi mengineyo (sawa na asilimia 36 ya lengo) **(Kiambatisho Nambari 1b)**.

### 2.7.2 Fungu G02: Programu ya Usimamizi wa Upatikanaji wa Haki

54. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Mahkama Kuu Zanzibar. Hadi kufikia Machi 2026, shughuli zifuatazo zimetekelezwa:

i. Jumla ya Mashauri 5,519 yamesajiliwa. Mashauri 2,847 yamepatiwa maamuzi sawa na asilimia 52 na Mashauri 2,672 yanaendelea kufanyiwa kazi. Ufafanuzi wa mashauri hayo upo katika **Kiambatisho Nammbari 4**;
ii. Vikao vya ushirikiano na wadau wa haki jinai katika ngazi ya Mahkama Kuu na Mikoa vimefanyika, na kusaidia kuongeza kasi ya usikilizaji wa mashauri na kuboresha malipo ya mashahidi. Aidha, elimu kwa umma imetolewa kupitia vyombo vya habari, maonesho na vipindi 36 vya televisheni vya 'IJUE MAHKAMA';
iii. Katika jitihada za kuongeza kasi ya usikilizaji wa mashauri, Mahkama imeandaa timu maalumu ya Mahakimu kusikiliza Mashauri ya Udhalilishaji kwa Mkoa wa Mjini Magharibi (Mazizini). Kambi hiyo ilianza kusikiliza mashauri kuanzia tarehe 23 Februari 2026 hadi tarehe 15 Aprili 2026, na jumla ya mashauri 85 yamesikilizwa na yanatarajiwa kumalizika kwa wakati;
iv. Mahkama ya Kadhi Zanzibar, kupitia Kadhi Mkuu, Makadhi na Maafisa, ilishiriki katika mafunzo ya kubadilishana uzoefu huko Mombasa nchini Kenya; na
v. Jumla ya Hati za Makubaliano mbili (2) zimewekwa saini baina ya Mahkama ya Zanzibar pamoja na Skuli ya Sheria, na Chuo Cha Mahkama Lushoto na Mahkama ya Zanzibar.

**55. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Mahkama Kuu ilipangiwa kutumia **Sh.15,287,800,000** (**Sh.10,205,700,000** mishahara na **Sh.5,082,100,000** matumizi mengineyo). Hadi Machi 2026, **Sh.10,575,176,545** zimepatikana (sawa na asilimia 69 ya lengo) ambapo **Sh.6,745,776,545** zilitumika kwa mishahara (sawa na asilimia 66 ya lengo) na **Sh.3,829,400,000** zilitumika kwa matumizi mengineyo (sawa na asilimia 75 ya lengo).

**56. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Miradi, **Sh.13,000,000,000** zilipangwa na **Sh.7,660,828,754** zimepatika sawa na asilimia 59 ya lengo. Mchango wa Serikali katika utekelezaji wa Mradi wa Maboresho ya Mahkama, **Sh.600,000,000** zimepangwa na **Sh.510,169,000** zimepatika. Aidha, Mradi wa Maboresho

ya Mahkama (Zi-JUMP) imepangiwa **Sh.35,000,000,000**. na **Sh.17,633,394,251** zimepatikana (sawa na asilimia 50 ya lengo) **(Kiambatisho Nambari 1b na 1c)**.

57. **Mheshimiwa Spika,** Mahkama ya Kadhi, ilipangiwa kutumia ruzuku ya **Sh.2,501,400,000** (mshahara **Sh.1,879,000,000** na matumizi mengineyo **Sh.622,400,000.** Hadi kufikia Machi 2026, **Sh.2,701,980,826** zimepatikana (sawa na asilimia 108 ya lengo) ambapo **Sh.2,285,180,826** zilitumika kwa mishahara (sawa na asilimia 122 ya lengo) na **Sh.416,800,000** zilitumika kwa matumizi mengineyo (sawa na asilimia 67 ya lengo).

58. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa mapato, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Mahkama ilikadiriwa kukusanya **Sh.1,277,267,000** hadi Machi 2026, **Sh.424,882,783** zimekusanywa (sawa na asilimia 33 ya lengo)

### 2.7.3 Fungu G03: Programu ya Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Sheria

59. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu. Hadi kufikia Machi 2026, Afisi imetekeleza shughuli zifuatazo:-

   i. Kanuni 22 zinazotokana na Sheria tofauti zimetayarishwa kwa lengo la kuzifanya Sheria hizo ziweze kutekelezeka kwa ufanisi zaidi. Sambamba na hilo, Afisi imeandaa jumla ya matangazo 107 ya Kisheria na kuyawasilisha kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji kwa ajili ya kuchapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali;

   ii. Jumla ya mikataba 429 ilitolewa ushauri, ikijumuisha Mikataba ya Bidhaa na Huduma 250, Mikataba ya Ujenzi 97, Mikataba ya Ushauri Elekezi 73 na Mikataba ya Kodi tisa (9). Aidha, Afisi iliendelea kutoa ushauri wa kisheria katika Hati za Maelewano (MoUs), ambapo jumla ya Hati za Maelewano 148 zilitolewa ushauri katika sekta mbalimbali;

   iii. Jumla ya kesi 19 zimefunguliwa Mahkamani. Kesi 16 zilisikilizwa na kumalizika, ambapo Serikali ilishinda kesi 15 na kesi moja (1) ilimalizika kwa njia ya makubaliano;

iv. Jumla ya Indhari 24 za kuishtaki Serikali zilipokelewa ndani ya kipindi cha Julai 2025-Machi, 2026;

v. Afisi imeendelea kufanya mapitio ya sheria kwa kufanya utafiti mdogo na kuandaa muhtasari wa Sheria za Zanzibar, ambapo Sheria 293 zimetayarishwa kwa muhtasari. Vilevile, Afisi imefanikiwa kuandaa rasimu ya awali ya Sheria ya Kupinga Ukatili wa Kijinsia;

vi. Jumla ya Wafanyakazi Wanne walipata fursa ya kuanza mafunzo ya muda mrefu katika kada ya Sheria na Uhasibu. Jumla ya wafanyakazi sita walipata fursa ya kushiriki katika mafunzo mbalimbali ya muda mfupi. Mafunzo haya yalihusu uhasibu, ukaguzi wa ndani, ufuatiliaji na tathmini pamoja na huduma bora za usafirishaji;

vii. Mawakili wa Serikali 12 wamepatiwa mafunzo ya kutumia Njia Mbadala za Kutatua Migogoro (ADR). Vilevile, jumla ya Wafanyakazi Sita (06) kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu walipata fursa ya ufadhili wa Mafunzo ya muda mfupi kutoka Ubalozi Mdogo wa India na Jamhuri ya Watu wa China katika maeneo ya usuluhishi wa migogoro na uandishi wa sheria; na

viii. Afisi ya Mwanasheria Mkuu Pemba imeweza kusimamia na kuiwakilisha Serikali Mahakamani katika mashauri 19 ya madai. Jumla ya kesi 11 zilimalizika na mashauri Tisa yaliondolewa Mahakamani. Katika kipindi husika, jumla ya indhari Sita za kuishtaki Serikali zilipokelewa na kufanyiwa kazi.

**60. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu ilipangiwa kutumia **Sh.6,962,700,000** (**Sh.3,632,900,000** mishahara na **Sh.3,329,800,000** matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi 2026, **Sh.3,058,856,538** (sawa na asilimia 44 ya lengo) zimepatikana ambapo **Sh.2,076,459,538** (sawa na asilimia 57 ya lengo) zimetumika kwa mishahara na **Sh.982,397,000** zimetumika kwa matumizi mengineyo (sawa na asilimia 30 ya lengo) **(Kiambatisho Nambari 1b)**.

### 2.7.4 Fungu G04: Programu ya Usimamizi wa Utekelezaji wa Kesi za Jinai

61. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Hadi kufikia Machi 2026, shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

i. Majalada 2,433 yanayohusisha makosa mbalimbali ya jinai yalipokelewa. Kati ya hayo, 451 yalihusu makosa ya udhalilishaji, 833 wizi, 460 shambulio, 264 uvunjifu wa amani, 40 rushwa na uhujumu uchumi, 20 mauaji, 138 dawa za kulevya, 173 usalama barabarani na 54 makosa mengineyo;

ii. Kesi 1,161 zimefunguliwa katika Mahkama mbalimbali. Kati ya kesi hizo, kesi 226 zimekamilika kwa washtakiwa kupatikana na hatia, kesi 68 zilipelekea washtakiwa kuachiwa huru, na kesi 98 ziliondolewa kwa sababu mbalimbali za kisheria. Kwa sasa, kesi 769 zinaendelea na zipo katika hatua mbalimbali za usikilizwaji Mahkamani;

iii. Kituo Jumuishi cha Kushughulikia Makosa ya Kiuchumi kinaendelea kushughulikia majalada 9 ya kesi za makosa ya kiuchumi. Aidha, mali za uhalifu zenye thamani ya **Sh.14,473,700,000** ikiwemo nyumba 15, viwanja 5 na magari 3 zimezuiliwa kupitia amri ya 'Prohibitory Notice', na mali za watuhumiwa zenye thamani ya **Sh.3,124,000,000** zikiwemo magari 11, viwanja 10 na nyumba 5 zimetaifishwa;

iv. Muongozo maalum wa kuyatambua makosa yaliyomo chini ya Sheria ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi, Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, na Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha Haramu umetayarishwa ili kurahisisha upelelezi na uendeshaji wa mashtaka. Aidha, Afisi inaendelea kushughulikia masuala yanayohusu makosa yanayovuka mipaka yakihusisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mataifa mbalimbali;

v. Ofisi, kupitia Kamati ya Kuzuia Udhalilishaji wa Kijinsia Zanzibar, imekamilisha kazi ya kubaini mianya inayopelekea udhalilishaji wa kijinsia pamoja na kupendekeza masuluhisho

yake ili kurahisisha utekelezaji kwa Serikali, sekta binafsi, Asasi za Kiraia na wanajamii;

vi. Ofisi iliendesha mafunzo mbalimbali ikiwemo kuwajengea uwezo watendaji wa Dawati la Msaada kwa Mashahidi ili waweze kuwahudumia mashahidi kwa ufanisi; kuwajengea uwezo wapelelezi, waendesha mashtaka na mahakimu kuhusu fedha mtandao (cryptocurrency), utakatishaji wa fedha haramu na kula njama kwa ajili ya kutenda makosa ya jinai. Aidha, madaktari 25 walijengewa uwezo kuhusu namna ya kumchunguza muhanga wa makosa ya udhalilishaji;

vii. Ofisi iliendesha mafunzo kuhusu matumizi ya Mfumo wa Ushughulikiaji Majalada ya Kesi za Jinai (Case File Management System - CFMS), ambapo jumla ya washiriki 145 kutoka ZAECA, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Jeshi la Polisi pamoja na waendesha mashtaka Unguja na Pemba walipatiwa mafunzo hayo. Kwa sasa mfumo huo umeanza rasmi kutumika; na

viii. Ofisi kupitia Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti kilidahili wanafunzi wapya 120 kwa mwaka wa masomo 2025/2026 ambapo jumla ya wanafunzi 78 kwa ngazi ya cheti na wanafunzi 42 kwa ngazi ya Diploma.

**62.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu hii ilipangiwa kutumia **Sh.7,255,800,000** (mishahara **Sh.5,415,200,000** na **Sh.1,840,600,000** matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi 2026, **Sh.3,908,129,954**. zimepatikana (sawa na asilimia 54 ya lengo) ambapo **Sh.3,363,169,996** zimetumika kwa mishahara (sawa na asilimia 62 ya lengo) na **Sh.544,959,958** zimetumika kwa matumizi mengineyo (sawa na asilimia 30 ya lengo). Aidha, ruzuku ya **Sh.228,600,000** imepangwa kutumika kwa uendeshaji wa Kituo cha Sheria, ambapo hadi kufikia Machi 2026, **Sh.71,315,800** zimepatikana (sawa na asilimia 31 ya lengo) **(Kiambatisho Nambari 1b).**

### 2.7.5 Fungu G12: Programu ya Haki na Uwezeshaji Kishariah

63. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, hadi kufikia Machi, 2026 shughuli zifuatazo zimetekelezwa: -

i. Kamisheni imeimarisha upatikanaji wa haki za mirathi na kuhaulisha umiliki wa mali kwa ndugu na jamaa wa wafiwa, ambapo jumla ya tirka 1,078 zimefunguliwa na tirka 1,065 zimefungwa na warithi kupewa haki zao. Tirka zilizofungwa zilikuwa na thamani ya fedha taslimu **Sh.19,340,524,482** majengo yenye thamani ya **Sh.12,711,508,383**, viwanja vyenye thamani ya **Sh.244,400,000** na mashamba yenye thamani ya **Sh.2,075,741,059**.

ii. Jumla ya kesi 53 zimesimamiwa Mahkamani. Kati ya hizo, kesi 9 ni mpya na 44 zinaendelea; kesi 7 zimeshatolewa hukumu, 44 zinaendelea na hakuna kesi iliyokatiwa rufaa. Kamisheni imetatua mizozo 47 iliyojitokeza katika uendeshaji wa shughuli zake, ambapo 25 ilihusu mirathi na 22 wakfu;

iii. Kamisheni imefanikiwa kutatua kadhia ya mirathi kwa Wazanzibari Waislamu wanaofanya kazi katika taasisi za Muungano au kufariki Tanzania Bara. Ufumbuzi rasmi umepatikana kupitia makubaliano maalum yaliyofikiwa kati ya Kamisheni na taasisi za Muungano zinazohusiana na maswala haya. Makubaliano hayo yataanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2026/2027;

iv. Kamisheni imeendelea kutunza, kusimamia na kuimarisha uhifadhi wa nyaraka na uwekaji wa mali za wakfu na amana ili kuongeza tija kwa wanufaika. Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, nyumba 132 na mashamba 7 yamekaguliwa. Kati ya mali zilizokaguliwa, nyumba 38 zinahitaji marekebisho, 49 masharti ya upangaji yapo sawa na 45 zinahitaji uangalizi wa karibu. Kodi ya **Sh.821,993,092** imekusanywa. Aidha, **Sh.33,335,934** zimetumika kutekeleza wasia;

v. Kamisheni imeendelea kuratibu shughuli za Hijja, Umra na Ziara, ambapo jumla ya mahujaji 4,036 wanatarajiwa kusafirishwa na

Taasisi 49 za Tanzania, zikiwemo 30 za Zanzibar na taasisi 19 za Tanzania Bara. Mahujaji wanaotarajiwa kusafirishwa na Taasisi za Zanzibar ni 2,636 na wanaotarajiwa kusafiri na taasisi za Tanzania Bara ni 1400; na

vi. Zaka, sadaka na misaada ya kheri yenye thamani ya **Sh.2,868,994,750** imegawanywa kwa jamii ya Zanzibar.

**64. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu hii ilipangiwa kutumia **Sh.2,762,000,000** (mishahara **Sh.1,828,100,000** na **Sh.933,900,000** matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi 2026, **Sh.1,680,755,255** zimepatikana (sawa na asilimia 61 ya lengo), kati ya fedha hizo, **Sh.1,311,070,099** zimetumika kwa mishahara (sawa na asilimia 72 ya lengo) na **Sh.369,685,156** zimetumika kwa matumizi mengineyo (sawa na asilimia 40 ya lengo). Aidha, Kamisheni ilikadiriwa kukusanya mapato **Sh.336,222,160** hadi Mwezi Machi 2026, **Sh.98,624,506** zimekusanywa (sawa na asilimia 29 ya lengo). **(Kiambatisho Nambari 1a na 1b)**

### 2.7.6 Fungu G14: Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini

**65. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar. Hadi kufikia Machi, 2026 shughuli zifuatazo zilitekelezwa: -

i. Madrasa 230, misikiti 120 na Maahad 1 zimekaguliwa kwa ajili ya kutoa miongozo ya uimarishaji wa taasisi hizo. Aidha, Ofisi imesajili madrasa 166 na misikiti 154;

ii. Jumla ya walimu wa madrasa 419 wamehitimu mafunzo ya uwalimu na kupatiwa shahada na leseni za kufundishia. Kati ya hao 159 ni wanaume na 260 ni wanawake;

iii. Ofisi imepokea migogoro 543 ya ndoa, 640 ya talaka na migogoro 158 inayohusu huduma za watoto, rejea, mirathi na kutelekeza. Migogoro hiyo imetatuliwa, mengine wahusika wameshauriwa waende mahakamani pamoja na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ili kutafutiwa ufumbuzi;

iv. Ofisi imefanikiwa kutangaza katika Gazeti Rasmi la Serikali 'Fatwa ya Talaka za Mitandaoni' na 'Fatwa ya Eda' ili kuiwezesha

jamii kuwa na uelewa wa mambo hayo. Ofisi imeendelea kutoa mafunzo ya ndoa kwa wananchi, ambapo jumla ya wananchi 398 wamepatiwa mafunzo hayo wakiwemo wanaume 136 na wanawake 262;

v. Ofisi inaendelea kutoa elimu na nasaha kwa wananchi. Jumla ya masuala 149 yanayohusu tohara, funga, ndoa, talaka n.k yamejibiwa kupitia njia ya redio na televisheni zinazomilikiwa na taasisi mbalimbali za Serikali na binafsi. Ofisi ilifanikiwa kurushwa vipindi 117 katika mitandao ya kijamii kupitia You Tube ya Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar, Face book na WhatsApp; na

vi. Ofisi iliratibu mashindano ya kitaifa ya Qur-ani na futari ya pamoja iliyowajumuisha wananchi kutoka mikoa yote ya Zanzibar, pamoja na kuimarisha ushirikiano wa kidini na jamii. Elimu ya maadili, amani na usalama kwa wanafunzi, vijana wa bodaboda na jamii mbalimbali, pamoja imetolewa; na

vii. Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar inaendelea na matayarisho ya ujenzi, uratibu wa kukipandisha hadhi Chuo cha Kiislamu kuwa chuo chenye kutoa elimu kuanzia cheti hadi digirii ya kwanza na kuongeza ufanisi wa mitaala na program za elimu zenye kukidhi mahitaji ya soko la ajira na mabadiliko ya kijamii yanayoendana na misingi na maadili ya Dini ya Kiislamu.

**66. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar ilipangiwa kutumia **Sh.2,819,200,000** (mishahara **Sh.1,407,900,000** na matumizi mengineyo Sh.1,411,300,000). Hadi kufikia Machi 2026, **Sh.1,763,456,277** zimepatikana (sawa na asilimia 63 ya lengo). Kati ya fedha hizo, **Sh.939,494,865** zimetumika kwa mishahara (sawa na asilimia 67 ya lengo) na **Sh.823,961,412** zimetumika kwa matumizi mengineyo (sawa na asilimia 58 ya lengo). **(Kiambatisho Nambari 1b).**

### 2.7.7 Fungu G15: Programu ya Usimamizi wa Maadili ya Viongozi

**67. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

i Fomu 2,979 za Tamko la Rasilimali na Madeni zimepokelewa na kusajiliwa, sawa na asilimia 104 ya makadirio. Kati ya Fomu hizo, Fomu 55 ziliwasilishwa na viongozi nje ya muda uliowekwa kisheria;

ii Tume imeendelea kuchukua hatua za kisheria kwa viongozi waliochelewa na walioshindwa kwa makusudi kurejesha Fomu za Tamko la Rasilimali na Madeni. Tume inaendelea kupokea fomu za viongozi wapya wanaopata nafasi za uteuzi kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Aidha, katika kukidhi matakwa ya kisheria, orodha ya majina ya viongozi wote waliowasilisha Fomu za Tamko la Rasilimali na Madeni kwa mwaka 2025/2026 imechapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali kupitia Tangazo la Kisheria Nambari 7439 la Mwaka 2026;

iii Jumla ya viongozi wa umma 217 (Unguja 173 na Pemba 44) wamehakikiwa, sawa na asilimia 94 ya lengo la viongozi 230 kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

iv Tume imo katika hatua za kutengeneza Dirisha la Mfumo (Public Leader's Self Service Portal - PLSSP) utakaowawezesha viongozi kujisajili, kujaza na kuwasilisha Fomu ya Tamko la Rasilimali na Madeni kwa njia ya mtandao (online submission). Kukamilika kwa hatua hiyo kutaiwezesha Tume kuchambua na kupata taarifa mbalimbali za kiutendaji, kurahisisha jukumu la uhakiki wa taarifa za viongozi na kuunganisha mifumo ya taasisi nyingine za Serikali, ikiwemo Wakala wa Matukio ya Kijamii (ZAN ID System), Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Watumishi na Malipo (HR-PayMIS), Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali, mifumo ya Mamlaka ya Mapato (ZRA Systems), Kamisheni ya Ardhi (Land Management System), na mifumo mingine inayohusika;

v Jumla ya malalamiko 16 ya ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi yamepokelewa na kufanyiwa kazi. Kati ya malalamiko hayo, malalamiko 6 yamekamilika na kutolewa uamuzi. Malalamiko 10 yapo katika hatua mbalimbali za uchunguzi.

Malalamiko hayo yanahusiana na matumizi mabaya ya madaraka, uasharati, ucheleweshaji wa utoaji wa haki, kushindwa kulipa deni, matumizi ya lugha isiyofaa, uwonevu na ugomvi;

vi Ripoti ya Tisa ya Utekelezaji wa Kazi za Tume kwa mwaka 2024/2025 ilitayarishwa na kuwasilishwa kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, tarehe 25 Septemba 2025 kwa hatua zake kwa mujibu wa kifungu cha 29(1) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Aidha, Ripoti hiyo iliwasilishwa mbele ya Baraza lako na kujadiliwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi katika Mkutano wa Pili wa Kikao cha Kumi na Mbili uliofanyika tarehe 26 Februari 2026; na

vii Tume ya Maadili, kwa kushirikiana na taasisi za Utawala Bora, iliadhimisha Siku ya Maadili na Haki za Binadamu tarehe 15 Desemba 2025, ikiwa na kaulimbiu *'Matumizi sahihi ya mifumo ya kidigitali huimarisha uwajibikaji, uadilifu, haki za binadamu na kudhibiti rushwa'.*

**68. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Tume ilipangiwa kutumia **Sh.2,558,200,000** (mishahara **Sh.1,209,400,000** na **Sh.1,348,800,000** matumizi mengineyo). Hadi kufikia Machi 2026, **Sh. 1,574,615,552** (sawa na asilimia 62 ya lengo) zimepatikana. Kati ya fedha hizo, **Sh.1,058,395,677** (sawa na asilimia 88 ya lengo) zimetumika kwa mishahara na **Sh.516,219,875** (sawa na asilimia 38 ya lengo) zimetumika kwa matumizi mengineyo **(Kiambatisho Nambari 1b)**.

### 2.7.8 Fungu E04: Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma

**69. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hadi kufikia Machi, 2026 shughuli zifuatazo zimetekelezwa: -

i. Miongozo ya Ukaguzi wa Kiuchunguzi (Forensic Audit Manual) na ukaguzi wa uzingatiaji wa sheria imeandaliwa;

ii. Mikataba ya kazi za ukaguzi (Engagement Letters) kati ya mkaguzi na mkaguliwa imeimarishwa;

iii. Ofisi imeshiriki katika ukaguzi wa balozi mbalimbali za Tanzania nje ya nchi, ikiwemo Marekani, Brazil, Namibia, Afrika Kusini, Zimbabwe na Comoro, kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT);
iv. Kukamilika kwa ukaguzi wa mafao ya fidia, pensheni na kiinua mgongo kwa mafanikio makubwa, ikiwa ni pamoja na kushughulikia jumla ya majalada 1,271 ya mafao ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na ZSSF;
v. Kuimarisha uwezo wa watumishi kupitia mafunzo ya kitaaluma, ambapo jumla ya watumishi wawili (2) wamefanikiwa kupata CPA na Watumishi wawili (2) wamepata CISA; na
vi. Ofisi imefanikiwa kukamilisha ukaguzi wa hesabu za Wizara, Mashirika na Miradi ya Maendeleo, hatua inayochangia kuimarika kwa uwajibikaji na usimamizi bora wa fedha za umma.

70. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu hii ilipangiwa kutumia **Sh.8,837,200,000** (mishahara **Sh.5,806,800,000** na matumizi mengineyo **Sh.3,030,400,000)**. Hadi Machi 2026, **Sh.5,609,279,860** (sawa na asilimia 63 ya lengo) zimepatikana. Kati ya fedha hizo, **Sh.4,498,828,110** (sawa na asilimia 77 ya lengo) zimepatikana kwa ajili ya mishahara na **Sh.1,110,451,750** (sawa na asilimia 37 ya lengo) zimepatikana kwa matumizi mengineyo. Aidha, Ofisi ilikadiriwa kukusanya **Sh.500,000,000.** Hadi Machi 2026, **Sh.223,589,000** (sawa na asilimia 45 ya lengo) zimekusanywa **(Kiambatisho Nambari 1a na 1b).**

### 2.7.9 Fungu E05: Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu Uchumi

71. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi, hadi kufikia Machi, 2026 shughuli zifuatazo zilitekelezwa: -

i. Mamlaka imefanya jumla ya mikutano 301 kwa taasisi za Serikali na binafsi pamoja na jamii katika shehia na skuli, kwa lengo la kutoa elimu juu ya madhara ya rushwa na uhujumu uchumi na kuimarisha ushirikiano na ZAECA. Aidha,

imeendesha kampeni za uelimishaji kupitia vipindi 17 vya redio na televisheni, maonesho 5, na kusambaza machapisho 3,580 ikiwemo vipeperushi, kalenda na dayari;

ii. Mamlaka imepokea tuhuma 465 za makosa mbalimbali, ikiwemo matumizi mabaya ya wadhifa na kukwepa kulipa kodi. Kati ya tuhuma hizo, majalada 26 yamefikishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kwa hatua za kisheria na majalada 4 yamewasilishwa Mahkamani. Pia, Mamlaka imefanikiwa kuokoa kiasi cha **Sh.5,480,187,032.88** na Dola za Kimarekani 203,135.84; kati ya hizo, **Sh.4,233,659,348.88** na Dola za Kimarekani 201,035.84 zilirudishwa Serikalini, na **Sh. 1,246,527,684** na Dola za Kimarekani 2,100 zilirudishwa kwa wananchi.

**72. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu hii ilipangiwa kutumia **Sh.10,871,800,000** (mishahara **Sh.8,473,700,000** na matumizi mengineyo **Sh.2,398,100,000.** Hadi kufikia Machi 2026, **Sh.5,354,909,687** zimepatikana (sawa na asilimia 49 ya lengo). Kati ya fedha hizo, **Sh.3,913,896,455** zimetumika kwa mishahara (sawa na asilimia 46 ya lengo) na **Sh.1,441,013,232** kwa matumizi mengineyo (sawa na asilimia 60 ya lengo) **(Kiambatisho Nambari 1b)**.

### 2.7.10 Fungu E07: Programu ya Usimamizi wa Watumishi wa Umma

**73. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Kamisheni ya Utumishi wa Umma, hadi kufikia Machi, 2026 shughuli zifuatazo zilitekelezwa: -

i. Kamisheni imepokea na kushughulikia mapendekezo ya Miundo kutoka katika Taasisi kumi. kati ya hiyo Miundo ya Taasisi minane na Miundo ya Utumishi miwili;

ii. Ukaguzi wa kushtukiza umefanyika kwa Taasisi za Umma thelathini na mbili (32) kwa lengo la kukagua utekelezaji wa masuala mbalimbali ya kiutumishi kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo ya Utumishi;

iii. Rufaa tatu (3) zimepokelewa na kufanyiwa maamuzi;

iv. Ripoti ya Mwaka ya Hali ya Utumishi wa Umma kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 imetayarishwa na kuwasilishwa Wizarani;
v. Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miundo ya Utumishi iliyoidhinishwa umefanyika kwa Taasisi za Umma ishirini na tano;
vi. Mkutano na Wakuu wa Taasisi za SMZ, Mashirika ya Umma, Wakala Tendaji, Mabaraza ya Miji pamoja na Halmashauri kwa upande wa Pemba, umefanyika kwa lengo la kuwakumbusha Wakuu wa Taasisi hizo juu ya umuhimu na wajibu wao wa kusimamia Utumishi wa Umma katika Taasisi wanazoziongoza;
vii. Vipindi vinne (4) vya Redio na TV (2 vya Redio na 2 vya TV) kuhusiana na kamisheni na majukumu vimetayarishwa na vimerushwa hewani kupitia ZBC. Aidha, kupitia vipindi hivyo wananchi waliweza kutoa michango mbalimbali na kuuliza maswali yanayohusu mada hizo;
viii. Jarida la Kamisheni Toleo la Pili limechapishwa na kusambazwa katika Taasisi mbalimbali za Umma na Binafsi; na
ix. Mafunzo juu ya utekelezaji wa Miundo ya Utumishi yametolewa kwa Taasisi sita (6) za SMZ.

**74. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamisheni ilipangiwa kutumia jumla ya **Sh.1,811,300,000**. Kati ya fedha hizo **Sh.1,052,200,000** ni kwa ajili ya mishahara na **Sh.759,100,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2026, **Sh.1,010,812,450** (sawa na asilimia 56 zimepatikana). Kati ya fedha hizo, **Sh.813,038,075** (sawa na asilimia 77) zimetumika kwa mishahara na **Sh.197,774,375** (sawa na asilimia 26) zimetumika kwa matumizi mengineyo). **(Kiambatisho Nambari 1b)**.

### 2.7.11 Fungu E08: Programu ya Usimamizi wa Uajiri, Haki na Nidhamu kwa Watumishi Serikalini

**75. Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Tume ya Utumishi wa Serikalini, hadi kufikia Machi, 2026 shughuli zifuatazo zilitekelezwa: -

i. Vibali vya ajira kwa watumishi 772 kati ya hao, 316 Wanaume na 456 Wanawake vimetolewa kwa Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali Unguja na Pemba. **(Kiambatisho nambari.5a)**;

ii. Idhini zimetolewa kwa Watumishi katika masuala mbalimbali ya kiutumishi ikiwemo: Watumishi 1,897 wamethibitishwa kazi, 1,421 wamepandishwa madaraja, 231 wamebadilishwa kada, 17 wameidhinishiwa nyongeza ya muda wa utumishi, na watumishi 44 wameidhinishiwa ajira za mkataba.**(Kiambatisho nambari 5b)**;
iii. Tume imeidhinisha kustaafu Watumishi kwa sababu mbalimbali ikiwemo watumishi wanne wamestaafu kwa hiari, watumishi 288 wamestaafu kazi kwa kufikia umri wa lazima na watumishi wawili wamestaafishwa kwa maradhi. Aidha, likizo bila malipo imetolewa kwa mtumishi mmoja na kutoa ruhusa ya kuacha kazi kwa hiari watumishi 7;
iv. Malalamiko mawili yamepokelewa na kuyafanyia kazi ambapo lalamiko moja mtumishi ametakiwa kurejea kazini au kuacha kazi na lalamiko la pili mtumishi amepatiwa uhamisho na kupangiwa kituo chengine cha kazi. Aidha, Tume imeidhinisha kufukuzwa kazi watumishi tisa (9) baada ya kupatikana na makosa ya kinidhamu, watumishi wawili wameacha kazi na watumishi wawili wameachishwa kazi; na
v. Mafunzo ya uelewa wa majukumu yametolewa kwa Wakurugenzi Utumishi, Maafisa Wadhamini na Maafisa Utumishi wa Wizara 17 na Taasisi zake.

**76. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Programu hii imepangiwa kutumia **Sh.1,375,000,000** (mishahara **Sh.733,100,000** na matumizi mengineyo **Sh.641,900,000**). Hadi Machi 2026, **Sh.866,379,366** zimepatikana, (sawa na asilimia 63 ya lengo). Kati ya fedha hizo, **Sh.561,780,787** zimetumika kwa mishahara (sawa na asilimia 77 ya lengo) na **Sh.304,598,579** zimetumika kwa matumizi mengineyo (sawa na asilimia 47 ya lengo) **(Kiambatisho Nambari 1b)**

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

77. **Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Ofisi ya Rais-Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha wa 2026/2027, imezingatia Mpango Mkakati wa Wizara 2024/2029, Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021/2026, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2050, Sera za Wizara na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) 2025/2030 pamoja na Mipango ya Maendeleo ya Kikanda na Kimataifa.

### 3.1 Vipaumbele vya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

78. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 OR-KSUUB imepanga kutekeleza bajeti kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo:

i. Kuendeleza matumizi ya Mifumo ya Kielektroniki katika Utumishi wa Umma;
ii. Kusimamia misingi ya utawala bora, maadili na kuongeza mapambano dhidi ya rushwa pamoja na Ukaguzi na Udhibiti wa Rasilimali za Umma;
iii. Kuendeleza ujenzi wa Tawi la Chuo cha Utawala wa Umma Pemba na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi, pamoja na kuanza ujenzi wa Skuli ya Sheria na Chuo cha Kiislamu;
iv. Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Urithishaji Viongozi (Succession Plan);
v. Kukamilisha na kuendeleza Miradi Mikubwa ya Ujenzi wa Miundombinu ya Mahkama;
vi. Kuanza utekelezaji wa Mikataba ya Uwajibikaji kwa Viongozi (Performance Contracts);
vii. Kuendeleza Programu za Mafunzo ya Kujenga Umahiri kwa Watumishi wa Umma;
viii. Kuratibu na kusimamia masuala ya dini pamoja na mali za amana;
ix. Kuendelea kuimarisha utendaji katika taasisi za Sheria na kufanya marekebisho ya Sheria mbalimbali; na

x. Kuendelea kuongeza uwelewa kwa jamii juu ya masuala ya msaada wa kisheria.

### 3.2 Malengo Makuu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**79. Mheshimiwa Spika,** ili kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele vya Ofisi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora imepanga kutekeleza malengo makuu yafuatayo: -

i. Kuimarisha upatikanaji wa haki na utawala wa sheria;
ii. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo ya Watumishi wa Umma kwa ajili ya upatikanaji wa Rasilimali Watu wenye sifa;
iii. Kuendelea kusimamia na kuratibu Programu ya Utekelezaji wa Mpango wa Mabadiliko ya Utumishi wa Umma PSRP II;
iv. Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika shughuli na utoaji wa huduma za Serikali na kukuza uchumi;
v. Kuimarisha misingi ya Utawala Bora, Uwajibikaji na maadili katika utendaji wa shughuli za Serikali; na
vi. Kuimarisha usimamizi na udhibiti wa rasilimali za Serikali pamoja na mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu uchumi.

### 3.3 Malengo ya Utekelezaji kwa Programu za Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**80. Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo haya sasa naomba kuwasilisha malengo ya utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kwa Programu za Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora.

**81. Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 itatekeleza malengo yake kupitia mafungu ya bajeti 11 na Programu Kuu 14. Malengo ya utekelezaji kwa kila Fungu la Bajeti na Programu kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 ni kama inavyowasilishwa hapo chini.

**82.** **Mheshimiwa Spika,** kati ya Programu hizi, Programu kuu nne (4) za Fungu 005 zitasimamiwa na kutekelezwa kupitia Idara zilizo chini ya Katibu Mkuu, na Programu Kuu 10 zitatekelezwa na Taasisi zinazojitegemea.

### 3.3.1 Fungu 005: Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora

**83.** **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora inasimamia Programu nne (4) na Taasisi mbili za ruzuku ambazo ni: -

**i.Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Sheria**

**84.** **Mheshimiwa Spika,** kupitia utekelezaji wa Programu hii, Idara ya Katiba na Msaada wa Kisheria kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 imepanga kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuratibu, kuendesha na kusimamia utoaji wa msaada wa kisheria pamoja na kuendeleza utekelezaji wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia Awamu ya Pili;
ii. Kutoa elimu kwa umma kwa kushirikiana na utoaji wa msaada wa kisheria kupita redio, televisheni na mikutano ya wazi;
iii. Kuratibu, kufuatilia na kutathmini kazi za utoaji wa Msaada wa kisheria; na
iv. Kuratibu na kushiriki vikao vya Katiba na Haki za Binadamu.

**85.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Idara imepangiwa kutumia **Sh.419,172,650** kwa matumizi ya kazi za kawaida na **Sh. 1,269,716,335** ikiwa ni ruzuku kutoka kwa wahisani **(Kiambatisho Nambari 2)**.

**ii. Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora**

**86.** **Mheshimiwa Spika**, Programu hii itatekelezwa kupitia Idara ya Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kufuatilia utendaji Serikilani kupitia utekelezaji wa Mikataba ya Utendaji Kazi wa Viongozi wa Wizara na Taasisi za Umma na kuwasilisha Ripoti za Tathmini katika Baraza la Mapinduzi.

Kupitia utaratibu huo, Mawaziri watasaini Mikataba ya Utendaji na Mhe. Rais na Kamatibu Wakuu na Viongozi wengine watasaini Mikataba hiyo kwa mujibu wa muongozo uliopo;

ii. Kurushwa hewani vipindi vya Utawala Bora, pamoja na masuala ya upatikanaji wa haki na utumishi kupitia televisheni mtandao (UB Online TV);

iii. Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mikataba ya Huduma kwa Mteja; na

iv. Kutayarisha Mpango wa kutathmini Taasisi za Umma kwa kutumia vigezo vya Utawala Bora.

**87. Mheshimiwa Spika,** Ili kuiwezesha Idara kutekeleza Programu hii kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, imepangiwa kutumia **Sh.565,329,300** kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida na mishahara. **(Kiambatisho Nambari 2)**.

**iii. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa ORKSUUB**

**88. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina maeneo mawili ya utekelezaji: eneo la uendeshaji linalotekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi, na eneo la uratibu linalotekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.

**a) Idara ya Uendeshaji na Utumishi**

**89. Mheshimiwa Spika,** Idara ya Uendeshaji na Utumishi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 imepanga kutekeleza yafuatayo:-

i. Kutoa huduma za kiutumishi na stahiki za kiutumishi kwa wafanyakazi wa Ofisi;
ii. Kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu, mfupi na mafunzo kwa vitendo;
iii. Kutoa huduma za kiuendeshaji kwa kuweka mazingira bora ya utendaji wa kazi; na
iv. Kuripoti matukio mbalimbali ya Wizara katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii pamoja na kuandaa mafunzo na kufanya matengenezo ya miundombinu na vifaa vya TEHAMA vya Ofisi.

**90.** **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Idara imepangiwa kutumia **Sh.3,273,200,400** kwa matumizi ya kazi za kawaida. (**Kiambatisho Nambari 2)**

**b) Idara ya Mipango, Sera na Utafiti**

**91.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

- i Kuratibu na kufanya mapitio ya Sera na Sheria zinazosimamiwa na Ofisi pamoja na Kuratibu na kuandaa nyaraka za kisera na kisheria zitakazowasilishwa Serikalini;
- ii Kuratibu utekelezaji wa mipango ya bajeti inayosimamiwa na Ofisi;
- iii Kutayarisha Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini pamoja na Mwongozo wa Takwimu wa Wizara kwa lengo la kurahisisha ufuatiliaji na kupima kiwango cha ufanisi wa majukumu ya Ofisi;
- iv Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Programu ya Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya Sheria na Programu ya Mpango wa Mageuzi ya Utumishi wa Umma wa Awamu ya Pili; na
- v Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Miradi inayotekelezwa na Ofisi. Miradi hiyo ambayo inatekelezwa kupitia ufadhili wa Mashirika ya Maendeleo ambao ni UNDP, UNWomen, Ubalozi wa Uingereza, Uswisi na Umoja wa Ulaya, ni pamoja na:-
    - a) Mradi wa Mfumo Endelevu wa Kupambana na rushwa Tanzania (BSAAT);
    - b) Programu ya Upatikanaji wa Haki kwa Wanawake na Wasichana katika Kukabiliana na Kesi za Ukatili Zanzibar; na
    - c) Programu ya Uwezeshaji na Upatikanaji wa Haki Kisheria Awamu ya Pili.

**92.** **Mheshimiwa Spika,** Ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, imepangiwa kutumia **Sh.466,223,878** kwa mishahara na matumizi ya kazi za

kawaida. Aidha, Miradi inayosimamiwa na Ofisi imepangiwa kutumia **Sh.1,717,577,037** kwa Mradi wa Upatikanaji wa Haki Kisheria, S**h.147,500,500** kwa Mradi wa Uwezeshaji Wanawake na Wasichana katika Kukabiliana na Kesi za Ukatili Zanzibar, na **Sh.3,184,801,563** kwa Mradi wa Mfumo Endelevu wa Kupambana na Rushwa Tanzania (BSAAT) **(Kiambatisho Nambari 2).**

***iv. Ofisi Kuu Pemba***

**93.** **Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu Pemba itaendelea kuratibu na kusimamia shughuli zote za utawala na utumishi, mipango na bajeti zinazotekelezwa na Ofisi kwa upande wa Pemba. Kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Ofisi Kuu Pemba imepangiwa kutumia **Sh. 737,446,450** kwa matumizi ya kazi za kawaida **(Kiambatisho Nambari 2).**

**v. Programu ya Uendelezaji wa Watumishi wa Umma.**

**94.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Usimamizi na Uendelezaji wa Watumishi wa Umma inatekelezwa na Idara ya Mipango ya Rasilimali Watu na Maendeleo ya Watumishi pamoja Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi.

***a) Idara ya Mipango ya Rasilimali Watu na Maendeleo ya Watumishi***

**95.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Usimamizi na Uendelezaji wa Watumishi wa Umma, Idara kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 imepanga kutekeleza kazi zifuatazo: -

i. Kufanya mapitio ya tathmini ya mahitaji ya mafunzo kwa Wizara, Idara na Wakala (MDAs);
ii. Kuendelea kufanya mapitio ya Mpango wa Rasilimali Watu wa Miaka Mitano (2026-2030), ambapo jumla ya watumishi wapya 7,500 wanatarajiwa kuajiriwa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Aidha, Idara itakamilisha Mfumo wa Tathmini ya Rasilimali Watu Zanzibar (ZHRAS) kwa lengo la kuweka idadi sahihi ya watumishi kwa taasisi zote za Serikali;
iii. Kuendeleza Mfumo wa Maombi ya Ajira Awamu ya Tatu (ZanAjira Phase 3) kwa lengo la kurahisisha zaidi mchakato wa

maombi ya ajira, na kuanzisha pamoja na kusimamia Mfumo wa Mafunzo kwa Utumishi wa Umma Zanzibar (Zanzibar Public Service Training System). Aidha, Idara itaandaa mifumo ya e-Loan, e-Likizo na Mfumo wa Huduma Binafsi kwa Watumishi (Employee Self-Service) ili mtumishi wa umma aweze kupata taarifa kwa wakati kupitia simu ya mkononi (mobile app);

iv. Kuandaa na kutekeleza programu za kujenga uwezo kwa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi wa Umma;

v. Kuandaa na kutekeleza Miongozo ya maendeleo ya taaluma (Career Progression); na

vi. Kuratibu programu za mafunzo zinazofadhiliwa na washirika wa maendeleo.

**96. Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Programu hii kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 imepangiwa kutumia **Sh.1,873,171,800** kwa matumizi ya kazi za kawaida. **(Kiambatisho Nambari 2)**.

***b) Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi***

**97. Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Programu hii kwa upande wa Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi, imepanga kutekeleza yafuatayo katika Mwaka wa Fedha 2026/2027:-

i. Kuimarisha Mfumo wa Taarifa za Watumishi na Malipo ya Mishahara (HR-PayMIS);

ii. Kufanya marekebisho ya Mshahara na Maposho kwa Watumishi wa Umma;

iii. Kuandaa Mfumo wa Upimaji Utendaji Kazi (PEPMIS) kwa Watumishi wa Umma;

iv. Kuimarisha mfumo wa upimaji wa utendaji kazi unaozingatia matokeo kwa watumishi wa umma;

v. Kuendelea kufanya mapitio ya Miundo ya Utumishi itakayolenga upandishwaji wa vyeo kwa matokeo na sifa;

vi. Kuendelea kufanya mapitio ya miundo ya taasisi kwa kuzingatia Hati Idhini ya Serikali ili iweze kukidhi mahitaji ya wataka huduma;
vii. Kufanya uhakiki wa Mishahara na Maposho (staff inspection) kwa watumishi wa umma; na
viii. Kuendelea kutoa Miongozo na Matoleo yanayohusu masuala ya utumishi.

98. **Mheshimiwa Spika,** Ili kuiwezesha Idara kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 imepangiwa kutumia **Sh. 1,412,845,500** kwa matumizi ya kazi za kawaida. **(Kiambatisho Nambari 2)**.

**Taasisi Zinazopokea Ruzuku**

99. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais - Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora inaendelea kusimamia Taasisi mbili zinazopokea ruzuku ambazo ni Chuo cha Utawala wa Umma (IPA) na Skuli ya Sheria.

**a) Chuo Cha Utawala wa Umma**

100. **Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Utawala wa Umma kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kimepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuandaa na kuendesha Programu za Mafunzo ya kuimarisha utendaji kazi kulingana na mahitaji yaliyopo katika Utumishi wa Umma;
ii. Kuandaa na Kuendesha Programu za Mafunzo ya awali kwa waajiriwa wapya wanaoingia katika ajira kwa mara ya kwanza;
iii. Kuendeleza ujenzi wa Tawi la Chuo cha Utawala wa Umma - Pemba;
iv. Kufanya tafiti katika Utumishi wa Umma ili kubaini mapungufu yaliyopo na kuandaa programu za mafunzo ya kujenga uwezo ili kuondoa kasoro zilizopo; na
v. Kuandaa na Kuendesha Programu za Mafunzo ya Muda mrefu kwa Watumishi wa Umma na wananchi wengine kutokana na mahitaji ya kiutumishi katika ngazi ya Shahada, Stashahada na Astashahada.

101. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Chuo kimepangiwa ruzuku ya **Sh.3,715,960,000** kwa ajili ya mishahara. **(Kiambatisho Nambari 2)**.

**b) Skuli ya Sheria Zanzibar**

102. **Mheshimiwa Spika,** Skuli ya Sheria Zanzibar kupitia Programu ya Mafunzo ya Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 imepanga kutekeleza kazi zifuatazo: -

i. Kuandaa Mafunzo maalumu kwa lengo la kuwajengea Uwezo Wasaidizi wa Sheria;
ii. Kuwepo kwa Mafunzo maalumu ya kuwaalika wageni wahadhiri (guest speakers) wa kuwasilisha mada kwa ajili ya kubadilishana uzoefu wao pamoja na wanafunzi wa Skuli;
iii. Kufanya utafiti wa masuala ya kisheria kwa kushirikiana na Sekta za Sheria; na
iv. Kutoa mafunzo ya sheria kwa vitendo kwa wahitimu wa vyuo vikuu (Mawakili) na wahitimu wa vyuo vya kati (Wasaidizi wa Sheria).

103. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Skuli ya Sheria imepangiwa kutumia **Sh.1,819,960,000** kwa ajili ya ruzuku ya matumizi ya kawaida na mishahara. Aidha, mapato ya **Sh.259,000,000** yanatarajia kukusanywa **(Kiambatisho Nambari 2)**

### 3.3.2 Fungu 026: Programu ya Usimamizi na Upatikanaji wa Haki Mahkama Kuu Zanzibar

104. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 imepanga kutekeleza kazi zifuatazo: -

i. Kuimarisha mazingira ya kazi na utoaji huduma za Mahkama
ii. Kuimarisha upatikanaji wa Haki
iii. Kuharakisha huduma za Mahkama na Usimamizi wa Mashauri
iv. Kukuza imani na uelewa wa jamii kuhusu kazi na utendaji wa Mahkama; na

v. Kuimarisha usimamizi wa utendaji, uhamasishaji wa rasilimali na uhusiano wa kimkakati na wahusika.

**105. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Mahkama Kuu imepangiwa kutumia **Sh.16,374,520,000**. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, Mahkama imepangiwa kutumia jumla ya **Sh.36,602,572,487,** kati ya hizo **Sh.1,600,000,000** zitatumika kwa Mradi wa Mchango wa Serikali katika utekelezaji wa Mradi wa Maboresho ya Mahkama na **Sh.35,002,572,487** Mchango wa Wahisani zitatumika kwa Mradi wa Maboresho ya Mahkama (Zi-JUMP). Aidha, Mahkama ya Kadhi imepangiwa kutumia Ruzuku ya **Sh.2,697,190,000** na **Sh.805,173,000** zinatarajiwa kukusanywa ili kuchangia mapato ya Serikali. **(Kiambatisho Nambari 1a, 1b, 1c na 2).**

### 3.3.3 Fungu 027: Programu ya Ukaguzi na Udhibiti wa Fedha na Rasilimali za Umma - Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

**106. Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 imepanga kutekeleza kazi zifuatazo: -

i. Kuimarisha ubora wa ukaguzi kwa kuzingatia na kutekeleza kikamilifu viwango vya kimataifa vya ukaguzi kwa taasisi kuu za ukaguzi katika sekta ya Umma (International Standards of Supreme Audit Institutions – ISSAIs) ili kuhakikisha uwajibikaji, uwazi na ufanisi wa kazi za ukaguzi;

ii. Kupanua na kuimarisha matumizi ya teknolojia katika ukaguzi (digital auditing), ikiwemo matumizi ya Akili Mnemba (AI), usalama wa mifumo ya TEHAMA (cybersecurity) pamoja na sayansi ya data (data science) ili kuongeza ufanisi na usahihi wa ukaguzi;

iii. Kuimarisha ukaguzi wa kiuchunguzi (forensic audits) na ukaguzi wa utendaji (performance audits) ili kubaini udanganyifu, ubadhirifu, na kupima ufanisi, tija na thamani ya fedha katika matumizi ya rasilimali za umma; na

iv. Kuendelea kuwekeza katika rasilimali watu kupitia mafunzo endelevu, kujenga uwezo wa kitaalamu na kuendelea kukuza

ujuzi wa watumishi ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya kisasa ya ukaguzi.

**107. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, Programu hii imepangiwa kutumia **Sh.9,811,860,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na mishahara. Ofisi imepangiwa kukusanya mapato ya **Sh.525,000,000**. **(Kiambatisho Nambari 1a na 2**).

### 3.3.4 Fungu 028: Programu ya Mageuzi ya Utoaji wa Huduma za Sheria- Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

**108. Mheshimiwa Spika,** Programu hii kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 imepanga kutekeleza yafuatayo:-

i. Kuimarisha Mfumo wa Sheria kwa kuandaa, kutayarisha, kuhifadhi na kusimamia masuala yahusuyo Uandishi wa Sheria, Kanuni na Matangazo ya Kisheria, kutoa ushauri wa Mikataba, kutoa ushauri wa kisheria katika Hati za Maelewano (MoUs);
ii. Kuiwakilisha Serikali Mahakamani dhidi ya Kesi zote za Madai, kufuatilia indhari za kuishtaki Serikali;
iii. Kufanya Uchambuzi na Ushauri katika masuala mbalimbali ya Kesi za Madai;
iv. Kushiriki katika mapatano, Utekelezaji na Ushauri wa Mikataba ya Serikali, Kikanda na Kimataifa, Kufanya Uchambuzi katika Uandishi wa Sheria;
v. Kufanya Utafiti na Mapitio ya Sheria za Zanzibar na kuzichapisha; na
vi. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kwenye Uandishi wa Sheria, Usimamizi wa Kesi, Masuala ya Mikataba na kuwajengea uwezo Maafisa wengine katika kada mbalimbali.

